

UTAMBULISHO WA KRISTO

KATIKA NYAKATI ZOTE



Hakika nayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa usiku wa leo. Ni mara yangu ya kwanza kuwa hapa katika jiji hili la kupendeza la Birmingham. Loo, nimetaka kuja, mara nyingi. Lakini inaonekana tu kana kwamba haitimii, Naye Bwana ana nyakati Zake Mwenyewe zilizotengewa mambo, kwa hiyo hivyo ndivyo ameyapanga. Tunashukuru kwa ajili ya wakati huu, na kwa ajili ya wadhamini hawa wazuri.

² Na sasa usiku wa leo kidogo ni...Daima sisi huwa na usiku wa ku—kufahamiana. Na, mwajua, wakati ukiwa katika jengo kama hili, ambamo kuna...halijatumiwa kwa ibada za kanisa, sidhani. Ninasikia kwamba ni ghala ya silaha. Labda ni la kwata tu, na kufanyia michezo, na kadhalika. Sio kama kuja kanisani. Ambako unaninii...Ninaamini ya kwamba kanisani mna Roho wa Mungu mle, na linaonekana kama ni hisi takatifu. Lakini unapokuja mahali ambapo kuna burudani, na wakati mwingine kufanya vituko, basi inaonekana kwamba kwa muda ni vigumu kuanza, mpaka tuzoeane. Halafu, basi, sote tukiwa hatufahamiani, mmoja kwa mwingine, inalifanya kwa namna fulani...Vema, tunaangalia na kushangaa. Lakini kama tukijaribu kuliondoa hilo, upesi tu iwezekanavyo.

³ Na—na kumbukeni tu tupo hapa kumtumikia Bwana Yesu. Tupo hapa kufanya tuwezalo, kila tuwezalo, kuuendeleza Ufalme Wake. Nami ninatoa jitihada zangu. Nami si—siwezi kufanya hilo peke yangu. Itahitaji msaada wenu na msaada wangu, na pamoja na msaada wa Mungu, na pamoja Naye tutaweza kuuona utukufu wa Mungu ukishuka na kutuzuru. Na hilo ndilo tunalotaka, hilo ndilo lililotuleta hapa, ni kuzuriwa na Mungu.

⁴ Sasa idadi yetu sio kubwa, wala hatuna umati mkubwa mno. Hatutakaa kwa muda mrefu sana. Na jambo lingine, mimi... Ujumbe wangu zaidi sana ni kwa watu wa full Gospel. Ni kwenye misingi yao, ingawa kila mtu huja.

⁵ Sisi huwaombea wagonjwa. Na hatudai kuwa mponyaji wala mtu anayeweza kumponya mwingine. Tunaamini ya kwamba kuna mponya mmoja tu, huyo ni Mungu. Bali tunaamini ya kwamba Yeye alimchagua mwanadamu kuwaombea wagonjwa, nasi hufanya hivyo. Tunawaombea wagonjwa. Naye Bwana ameturehemu, kuyajibu maombi yetu, mara nyingi sana. Nasi, kote ulimwenguni, tumeona, vema, kukiongezeka tu maelfu mara maelfu ya watu, viwete, wanaoteseka, vipofu, wasiojiweza,

vilema, wakiponywa. Nasi tunaamini tu ya kwamba tunaninii tu...kwamba, "Amejeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Nasi tunaamini ya kwamba hiyo ni fadhila, hayo ni majaliwa, kwa waaminio.

⁶ Sasa, si kwa wasioamini. Watu husema, "Vema, si—siamini hilo linaweza kutukia." Vema, kamwe halitatukia kwako. Jua—jua tu yakini, kamwe halitatukia kwako. Bali litatukia kwa hao waaminio, kwa kuwa ni kwa waaminio pekee.

⁷ Sasa hilo halitufanyi mponyaji, si zaidi ya vile kuhubiri wokovu kunavyotufanya Mwokozi. Tu—tunajua ya kwamba kuna mponya mmoja na Mwokozi mmoja, na huyo ni Mtu yule yule, Yesu Kristo. Tupo hapa kumtukuza kwa watu.

⁸ Sasa, uamsho hasa sio kuongezea wafuasi wanya kanisani. Uamsho ni kuamsha kile mlichio nacho tayari. Nami wakati mwingine nimeshangaa uamsho ni wa nini.

⁹ Hili huenda likasikika kidogo ni la kigeni, kwa mgeni kwenu, kusema hili. Lakini nilikuwa nimesimama ufukoni mwa ziwa, siku moja, huko Ziwa Michigan. Nilikuwa nikiyaangalia mawimbi, jinsi yanavyokuja na kurudi, nayo yangerushwa juu. Loo, upepo mkali ulikuwa ukivuma, na—nayo mawimbi yangerushwa juu sana hewani, na kuvurugavuruga juu chini, na kuviringika kisha yanarudi, tena yanakuja yakiviringika. Nikawaza, "Jamani, ni uamsho wa jinsi gani!" Lakini, mwajua, hakuna maji zaidi kwenye ziwa hilo kuliko kulivyo wakati limetulia kabisa na ni kimya. Hiyo ni kweli. Lina kiasi kile kile tu cha maji. Mnaona?

¹⁰ Basi ninashangaa, ni kwa nini ziwa hilo lote limevurugika hivi? Jinsi tu tunavyochochewa katika uamsho. Tunavurugika. Mnajua yanavyolifanyia hilo ziwa sikuzote, basi? Hulisafisha. Yanafagilia takataka zote ufukoni. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu hatuna budi kuwa na uamsho; kuondolea mbali kutokuamini kote na kadhalika kutoka kwetu, tupate kuona kwa udhahiri zaidi kile Mungu anachotutakia. Hilo ndilo tunalotazamia wakati huu, ni uamsho miongoni mwa watu.

¹¹ Sasa, mdhamini wangu, Ndugu Urshan, hawa ndugu hapa, na labda wengine wanaoketi huko ndani. Sasa, hao ni wahudumu wa Mungu, kama vile tu mimi na wahudumu wengine wote. Na ninii...

¹² Yesu alisema, wakati mmoja, "Ufalme wa Mbinguni umefananishwa na mtu aliyechukua jarife akaenda ziwani. Basi alipolitupa jarife ndani, alilivuta, na mle ndani alikuwa na wa kila aina." Jarife la Injili hushika wa kila aina, sasa, kila aina ya samaki. Mnaona, walikuwa labda baadhi yao walikuwa, tuseme, walikuwa mbwamaji, wengine walikuwa ni nyoka, wengine walikuwa ni buibui, wengine kasa, na—na kadhalika, na baadhi yao walikuwa ni samaki halisi. Kwa hiyo, hatujui tunachoshika katika jarife, tunavua tu.

¹³ Na sasa naja...Majuya mawili yatafika mbali zaidi ya juya moja, nami naja kuingiza jarife langu. Ni juya. Ndivyo tunavyoliita, huko Kaskazini ya mbali, *juya*. Nami naja ku—kuunganisha jarife langu pamoja na majarife yao, majarife yenu. Basi acheni tuyatupe huko mbali sana, mbali tuwezavyo. Na tuweke majarife yetu pamoja, na mioyo yetu pamoja, na juhudi zetu pamoja, na hebu tuvute, tuone kama kuna samaki ambao Bwana anaweza kuwatumia. Naye Ndiye anayeamua hilo. Sisi hatujui. Wote wanaonekana wamefanana kwetu. Wameshikwa tu kwenye jarife. Ila Mungu anajua hao ni nani, na aliwajua tangu mwanzo. Kwa hiyo sisi ni wavuvi tu, sisi si mahakimu wa kuamua ni nani aliye na ni nani asiye. Tunavua tu, kwa hiyo nipo hapa kuwasaidia.

¹⁴ Na sasa juma hili, omba, shika simu, mpigie simu mtu fulani, na uwaalike humu kanisani, hapa kwenye ghala ya silaha. Tuna muda mfupi tu. Wasiwasi, inawafanya watu kushikwa na wasiwasi inapofikia wakati tu wa kuzoeana, na watu kutulia, halafu inakubidi kwenda mahali pengine.

¹⁵ Mara nyingi nimeshangaa, wakati mwingine, kama—kama nisingeweza, moja ya siku hizi, kuwa na hema na nije huku kwenye jiji kubwa kama hili na kulitundika, kusudi tukae majuma kadhaa; na kufanya mkutano wa wahudumu asubuhi, na kukutana na wahudumu wote na kujadili jambo hilo.

¹⁶ Nami natumaini Bwana atazibariki jitihada zetu juma hili. Natumaini hakutakuwako na machela moja, wala kiti cha magurudumu, chochote kile, kitakachosalia hapa; wala mgonjwa mmoja aliye na matatizo ya moyo, TB, kansa; ila kile kitakachoponywa na Bwana Yesu. Nitakuwa nikiomba.

¹⁷ Sitembei sana, kwa kuwa, mwajua, huduma ya namna hii. Si kwamba sitaki kutembea. Lakini ni kwamba si—si—siwezi kumtumikia Mungu halafu mwanadamu, wakati ule ule. Sina budi kukaa peke yangu na kuomba. Nami nitakuwa nikifanya hivyo kwa ajili yenu. Nanyi mwe mkitekeleza sehemu hiyo nyingine, mkikusanyika na kuwaleta watu, na kadalika, na kuwaleta wagonjwa na wanaoteseka; na kuniombea, kila mmoja aniombee. Hivyo ndivyo tunavyopata ushindi.

¹⁸ Sasa ili tu kuweka msingi wa yale tunayojaribu kufanya. Sisi, kwanza, hatuwakilishi dhehebu lolote; hatulipingi dhehebu lolote, bali ni kwamba kamwe hatuwakilishi lolote. Tunasimama...

¹⁹ Niliwekwa wakfu, Mbaptisti wa Kimishenari. Halafu nikairudisha kadi yangu ya ushirika, sio ushirika na ndugu zangu, ni kusudi tu nisiwakilishwe miongoni mwa makundi yoyote. Nilikuja kwa Wapentekoste, hapo nilipoanza kuwaombea wagonjwa na kuagizwa kufanya hivyo. Nilikuja humu miongoni mwa Pentekoste, basi nikaona, nilifikiri walikuwa ni kundi moja tu, bali nikakuta kuna makundi

mengi kule kama ilivyo kwa Baptisti, makundi mbalimbali. Kwa hiyo ni—nikaona walikuwa wakizozana, na walikuwa wakizozana katika Baptisti, kuhusu *hili, lile, na linginelo*, kwa hiyo nikawaacha tu wazozane.

²⁰ Nami nitajaribu kumkumbatia kila mtu, na kusema, “Sisi sote ni ndugu. Hebu na tumtumikie tu Bwana.” Na ushawishi mdogo ninaoweza kuwa nao, siuweki juu ya dhehebu lolote lile, ni juu ya Kristo tu. Na hapo sisi. . . Nasi tunajaribu kumtumikia namna hiyo.

²¹ Kila mtu amelikwa, haidhuru. Kila mtu amekaribishwa. Mradi tu utakuwa na mwenendo mzuri na kuwa mtulivu, mbona, umekaribishwa vizuri iwezekanavyo.

²² Sasa, jambo lingine, ni mfumo wetu wa kuwaombea wagonjwa. Sasa, kila siku, Ndugu Borders, ama Terry, ama Ndugu Sothmann, ama Billy Paul ama . . . Kwa kawaida, ni Billy Paul. Hiyo ni kazi yake. Na kama hawezi kufika hapa, itakuwa ni mmoja wa watu hawa wengine atakayekuwa akizisambaza kadi za maombi kila siku. Wanafanya hivyo; wanashuka wanakuja, wanazichukua kadi za maombi, mia moja za hizo, na kuzichanganya, papo hapo mbele ya macho yenu, kisha wanawapa watu hizo kadi, wanaotaka moja. Sasa kila siku wanafanya hivyo. Ili kwamba, wakati tulipoanza kwa mara ya kwanza, tulikuta kwamba ilikubidi kuwa na kadi za maombi. Sio uwanja wa michezo, mwajua, kusukumana. Ni . . . Inakubidi kuwa na utaratibu.

²³ Halafu pia tukampata mtu mmoja akijaribu kuuza kadi za maombi, na kuwahakikishia watu watapanda, jukwaani. Na kwa hiyo, hilo, ilibidi tukomeshe hilo. Ndipo basi nikamweka mwanangu mwenyewe hapo, maana nilijua hataua hata moja.

²⁴ Ndipo wazo likazuka, “Nipe kadi fulani ya maombi. Utaanzia wapi kuwaombea, usiku wa leo? Halafu ni—nitaomba. . . Ninataka kadi hiyo ya maombi.” Vema, kuhakikisha kwamba mvulana huyo, la, hajui mahali mstari huo wa maombi utakapoanzia, yeye huzichanganya kadi, kisha anakupa. Hajui ni ipi anayokupa. Anakupa tu kadi ya maombi. Mtu anaweza akapata namba moja, mwingine hamsini, na—na halafu kadhalika.

²⁵ Halafu basi kulihakikisha hilo maradufu, mimi huja usiku, na hakuna mtu, wala mimi sijui, mimi mwenyewe, mahali nitakapoanzia kuziita hizo kadi za maombi. Huenda nikaanzia kwenye moja, pia huenda nikaanzia kutoka ishirini na tano. Huenda nikaanzia kwenye sabini na tano ama mia moja, na kurudi kinyumenyume; kumi na sita, na kwenda kimbelembele kisha kinyumenyume. Mtu yeyote ambaye amekuwa mkutanoni, anajua sisi hufanya hivyo, nyuma tu na mbele, popote pale.

²⁶ Na, halafu, kila siku. Kwanza, tunashuka tunaenda na kusambaza kadi zote za maombi, siku ya kwanza; basi wageni

wowote wakija, wanakosa kupata kadi ya maombi, hilo latosha, hawakuombewa kwenye mkutano. Lakini sasa tunazisambaza, kila siku, kusudi kila mtu anayetaka kadi ya maombi aweze kuipata. Labda usiku mmoja hatuzifikii zote, lakini, shikilia kadi yako, tutaifikia kabla ya kuondoka.

²⁷ Sasa, lakini kuna wengi, wengi wanaoponywa katika wasikilizaji, wengi zaidi wanaoponywa kuliko wakati wakiwa hapa jukwaani. Imani yako ndiyo inayoponya. Sio maombi yetu. Maombi yetu yatasaidia, hapana shaka. Sote tukiungana, tukuombee, itasaidia. Na kama . . .

²⁸ Halafu basi Jumapili alasiri, Bwana akipenda, tutamwombea kila mtu, tukichukua kadi zao za maombi na kuwaombea wote; ama labda Jumamosi usiku, mojawapo, inategemea ni ipi ndugu wanataka tufanye hivyo.

²⁹ Na sasa tunataka kusema jambo hili kusudi mweze kufahamu. Sababu ya mimi kuachana na mstari huo wa maombi, kukutana na kila mtu, ni kwa sababu kanuni zangu, ku—kusudi langu, ni hili, kwamba watu watampokea Kristo kama mponya wao pasipo mtu kuwawekea mikono.

³⁰ Kwa kawaida, ukimchukua mwinjilisti, anayekuja mjini, vema, yeye ni—yeye ni kila kitu katika kanisa hilo. Anapoondoka, wakati mwingine kusanyiko humwangalia mchungaji wao, na kusema, “Vema, vipi kuhusu mchungaji wenu ni mtuwa, nami nawatakeni mwe na heshima na mjue ya kwamba mtu huyo amewekwa wakfu kuwaombea wagonjwa kama tu vile mtu mwingine yeyote alivyowekwa wakfu. Nasi tu—tunawatakeni . . . na—na kwa . . .

³¹ Jambo lingine, kusudi letu, kuu, ni kwenu kuuona Uwepo wa Yesu Kristo, na kujua ya kwamba Yeye yupo hapa. Ndipo basi, wakati mkiwa katika Uwepo Wake, mkubalini tu kama Mwokozi na Mponya wenu. Iwapo hujaokoka, mkubali kama Mwokozi. Ikiwa umeokoka, na hujaponywa, basi mkubali kama Mponya wako. Ndipo hakuna mtu anayeweza kusema, “Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono.” La. Wewe uliweka mikono juu Yake, basi hilo ndilo jambo muhimu. Sasa nawatakeni mkumbuke hilo, wakati wote. Ni wewe kuweka ninii yako . . . kumgusa Yeye. Nayo Biblia ilisema, kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Na sasa kumbukeni hilo, ni wewe ukimgusa. Sio . . .

³² Mchungaji anayo haki ya kuwekea mikono. Kuweka . . . Sio tu mchungaji. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” waaminio tu, mtu yeyote anaweza kuwekea wagonjwa mikono, ana haki ya kufanya hivyo. Ni kujitambulisha na mtu huyo, katika maombi. Ni kama tu wewe unaweka mikono yako, kwa imani, juu ya Kristo, na kujitambulisha na Dhabihu yako. Kwa

hiyo kumbuka hilo sasa ju—juma linapoendelea, na uombe kwa uaminifu.

³³ Sasa, nafikiri hilo ni kama linayamaliza yote sasa. Na halafu kila usiku tunajaribu kuondoka mapema, mapema tu tuwezavyo. Sasa, tunaanza sasa kwenye saa tatu kasoro dakika ishirini na tano, kwa saa yangu ya mkono. Na Bwana akipenda, tunataka kutoka kila usiku kwenye saa tatu u nusu, ama labda mapema, kusudi mpate wakati wa kutosha, kwenda manyumbani mwenu kisha mrudi. Sasa kama hamjaombewa, ama hutaipata usiku wa kwanza . . .

³⁴ Huduma yangu huenda ikawa kidogo ni ya kigeni kwenu. Lakini ikiwa ni ya kigeni, usiitupe tu kando. Ketu ukaitafakari; ichukue Biblia. Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hakuyaandika hapa katika Biblia, bali ninamtaka aninii tu. . . Kama atadumisha tu yale aliyoandika *Humu*, yataniridhisha.

³⁵ Maana, tunaishi katika siku za kila namna ya vitu vigeni, itikadi ambazo si za kimaandiko. Lakini, mwajua, katika siku za Nuhu. . . Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Mwajua, watu labda walijenga mitumbwi katika siku hizo, kama zilijengwa na Mungu au la, bali hazikuelea wakati ulipowadia wa kuelea. Kwa hiyo ninapenda Ujumbe uwe umejengwa na Mungu kwa Maandiko, Ujumbe wa Kimaandiko, na papo hapo pamoja Nao, kila kitu pamoja na Maandiko. Ni BWANA ASEMA HIVI, basi. Nalo halina budi kusimama, kwa sababu, silo neno langu linalojadiliwa, litakuwa ni Neno Lake linalohojiwa. Lilete kutoka kwenye Maandiko!

³⁶ Nasi tuko katika muda wa wakati unaobadilika. Tunabadilika sasa. Na kila badiliko, kama tu kujenga jengo, unapofika kwenye kona, huna budi kupiga kona hiyo, ni—ni la kigeni. Kila mtu anataka kuendelea moja kwa moja; ungekuwa na ukuta mmoja mrefu. Bali tunajenga jengo. Nasi tumefika kwenye kona, nawe huna budi kubadilisha, kona hizo. Kama vile Ndugu Don Price alivyoinii vizuri sana, yeye. . . na jinsi alivyoweka vizuri sana si muda mrefu uliopita. Kwenye mabadiliko hayo ndipo matatizo yanapotokea, ambako ninii. . . Ni vigumu kwenye kona hiyo, kuifanya, kuikata kona hiyo na kuifanya ipasavyo kabisa.

Sasa kabla tu hatujalisoma Neno. . .

³⁷ Kila usiku, Ndugu Borders ndiye meneja wa mambo ya nje, naye pia huzungumza jukwaani.

³⁸ Naye Daktari Lee Vayle yupo hapa mahali fulani. Nadhani alifika huku. Alikutana nami huko Kentucky, nikiendesha maili thelathini kwa saa, nikiendesha Ford nyingine. Na kwa hiyo, nilipokuwa nikishuka, nilikutana naye. Naye ni m—mtu wa uhusiano. Atakuwa akizungumza, nadhani, mahali fulani mkutanoni, kila siku. Kwa hiyo kukiwako na maswali yoyote

ama chochote kile, mbona, mwulizeni Ndugu Vayle, ataweza kuwasaidia katika maswali haya. Vema. Sasa wakati sisi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

³⁹ Kabla hatujalisoma Neno, nina desturi kwamba tunasimama tunapolisoma Neno la Mungu. Sisi husimama tunapoimba *Bendera Iliyopambwa Nyota*, na kutoa heshima, mbona tusisimame tunapolisoma Neno la Mungu!

⁴⁰ Nitasoma usiku wa leo kutoka katika Waebrania, mlango wa 13, kuanzia kifungu cha kwanza.

Upendano wa ndugu na udumu.

Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.

Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili.

Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.

Mazungumzo yenu yasiwe ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo, kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.

Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini.

Wakumbukeni wale waliokuwa... wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao.

Yesu Kristo ni yeye yule jana, ... na leo na hata milele.

⁴¹ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, kwa ajili ya maombi. Sasa huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, sijui tu kama kungekuwako na haja usiku wa leo, mngetaka zikumbukwe, naomba mumwinulie Mungu mikono yenu, msembe, kwa hilo, "Nikumbuke, Ee Bwana." Asanteni.

⁴² Baba yetu wa Mbinguni, tunapokikaribia Kiti Chako cha Kiungu, katika Jina litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, ambaye alisema, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa." Nasi tunashukuru sana kwa ajili ya ahadi hiyo, tukijua jambo hili, ya kwamba imani yetu inasonga mbele sasa hivi kupita shaka lolote, tukijua kwamba sisi, kwa imani, tunazungumza ana kwa ana na Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa, ni ahadi. Na tena lilisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nipo papo hapo katikati yao."

⁴³ Sasa kila mmoja wetu ana haja, Bwana, kama vile tulivyoinua mikono yetu Kwako. Wewe unajua yaliyo mioyoni mwetu, chini ya mkono wetu. Nasi tunaomba ya kwamba

utatujibu, Bwana. Sio kwamba tunastahili kujibiwa, bali kwa sababu Wewe uliahidi kujibu. Ulisema ungetujalia. Nami najua utalifanya, kwa kuwa Wewe ni—Wewe Ndiye Mungu Mkuu aliyeziumba mbingu na nchi, na Hakimu wa mbingu zote na nchi. Na je! ungesema jambo ambalo usingelifanya sawa? Na iwe mbali na Mungu kufanya kitu kama hicho. Kinachokosekana, ni imani yetu kuliadini.

⁴⁴ Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba usiku huu uta—utaichochea sana imani yetu na kuisukuma kufikia mahali ambapo tutatembea pamoja nayo, Bwana, kupita ufahamu. Kwamba, hatutajaribu kufahamu; tutaadini tu. “Nayo imani ni kuwa na hakika ya mambo tunayotarajia, na ni bayana ya mambo tusiyoweza kuona wala kuthibitisha.” Tunaadini tu, na ni . . . Mungu huyafanya yatukie.

⁴⁵ Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba hapo, kwamba—kwamba Malaika wa Bwana watasimama kwenye kila mlango, na kila mstari wa viti, na kwenye—kwenye kila kiti; na atawasadikisha wenye dhambi, kwamba—kwamba wao, wao wa—wamekosea, na wajalie wampokee Bwana Yesu, basi. Na hao wasio na ubatizo wa Roho; jalia Roho Mtakatifu ashuke wakati tukizungumza, na wakati Uwepo wa Kristo ukiwa ni halisi sana. Tujalie, Bwana. Tunaomba ya kwamba hapatakuwapo na mnyonge miongoni mwetu. Jalia kila mtu anayeingia kwenye milango hii, Bwana, avuviwe sana kwa imani hata wataponywa, kila mmoja.

⁴⁶ Wabariki wahudumu hawa, Bwana, makanisa haya kote nchini. Jalia, kwa sababu ya jitihada hii kuu ambayo watu hawa wamefanya . . . Sisi ni watu wadogo, lakini, hata hivyo, Bwana, watu ambao ni waaminifu na wanajaribu kuishikilia Imani hiyo iliyokabidhiwa watakatifu mara moja, katikati ya giza. Jalia uje uamsho wa mtindo wa kale, hiyo ni kusema, utakaoenea kwenye makanisa haya kila mahali, na watakatifu wenye njaa waanze kulia, na wenye dhambi wazaliwe katika Ufalme wa Mungu, kama watakatifu. Tujalie, Bwana. Hilo ndilo kusudi letu. Hilo ndilo lililo mioyoni mwetu. Tunajaribu kufanya jambo hili kwa ajili ya heshima Yako, Bwana, kwa kuwa tunajua ya kwamba hatuna wakati mwingi mno wa kukaa.

⁴⁷ Tunaona dunia ikitikisika na kutetemeka tena, na kwenye Ijumaa Kuu, kama ilivyofanya miaka elfu moja mia tisa iliyopita kwenye Ijumaa Kuu. Nawe ulisema kutakuwako na matetemeko ya nchi mahali mahali. Tunaona ishara zote zikitokea, nasi tunajua wakati umekaribia.

⁴⁸ Kwa hiyo, Bwana, tunataka kufanya kazi wakati tukiweza, kwa kuwa, wakati uhai utakapokwisha, hatutafanya kazi tena. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba tutatoa jitihada zetu kwenye wakati huu. Ndipo wakati mkutano utakapokuwa umekwisha, jalia tujisikie kwamba tumefanya vizuri tuwezavyo. Tujalie, Bwana. Wabariki ndugu zangu, kila mahali. Wabariki

wote sasa watakaokuja mkutanoni, na hao watakaosikia. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi. Asante, ndugu.

⁴⁹ Ninataka kuchukua somo usiku wa leo, kama tu ningeliita somo, mazungumzo madogo rasmi, na kuyaita, Yesu. . . Yule Kristo, hasa, anatambulishwa katika nyakati zote. Kwa maneno mengine: *Utambulisho Wa Kristo Katika Nyakati Zote*.

⁵⁰ Kwa sababu, Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nasi tunataka ku—kuona, jinsi ambavyo katika nyakati zilizopita, kile Yeye alichokuwa. Sasa, tunazungumza sana kumhusu Yeye, na hilo ndilo limetuleta hapa sasa ni kuzungumza juu Yake. Na sasa, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na—na kama alionekana na kujulikana jana, basi kwa nini si leo hii? Kama alionekana na kujulikana, na kutambulishwa katika siku zilizopita, basi kwa nini sisi tusifanye jambo lile lile leo hii?

⁵¹ Tunaona, Mtu huyu mkuu, hakuna mtu angaliweza kusikia habari Zake pasipo wao ku—kutaka kujua mengi zaidi kumhusu. Kuna jambo fulani kumhusu! Jina hilo la Yesu Kristo, hakuna kabisa jina lingine, popote, linalowavutia watu kama hilo. Kuna jambo fulani kuhusu Hilo!

⁵² Mtu, ni, anajua yeye anatoka huko ng'ambo. Na uvuli mweusi wa pazia unaoning'inia kati yake na mahali alipokuwa kabla hajaja huku, naye anajua hana budi kwenda nyuma ya pazia hilo. Na daima anataka kujua mahali alikotoka, na kwamba yeye ni nani, na mahali anakoenda. Tuna mamilioni ya vitabu ambavyo vimeandikwa, nakisia, juu ya somo hilo. Bali kuna Kitabu kimoja tu, na hicho ni cha. . . Hicho ni vitabu sitini na sita ndani Yake, ambavyo vinaweza kukwambia mahali ulipotoka, kwamba wewe u nani, na mahali unapokwenda, na hicho ni Biblia hii. Neno ndilo linalokwambia unakotoka, wewe ni nani, na unakoenda.

⁵³ Watu wengi sana wana mawazo mengi mbalimbali kumhusu Kristo, na hasa sana katika siku hii tuliyo nayo sasa.

Tunao wengine wao wanaomchukulia tu kama mwalimu mkuu.

⁵⁴ Na, Yeye alikuwa hivyo, bali alikuwa ni zaidi ya mwalimu mkuu. Mnaona? Alikuwa hivyo. Hapajakuwapo na mtu aliyenena kama Yeye, bali alikuwa ni zaidi ya mwalimu mkuu tu. Lakini hiyo inaonekana kuwa kama falsafa kuu miongoni mwa mengi ya makanisa leo hii, kumchukulia tu kama mwalimu, ambaye hajapata kufundisha kama Yeye hapo kabla. “Yeye ni mwanahistoria mkuu wa kale, wa ajabu sana, ama mwalimu, hasa, wa siku zilizopita. Mafundisho yake ni mazuri, na unaweza kuamini sehemu yake, na sehemu yake huwezi. Lakini alikuwa ni mwanafalsafa kwelikweli!” Kwa maneno mengine, wanamhesabu kitu kama Confucius, mwanafalsafa M—Mchina

wa mamia mengi ya miaka iliyopita. Sasa, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwalimu. Yeye ni—Yeye ni zaidi ya huyo.

Kisha wengine, juu Yake, wanamdhania kwamba ni mtu mzuri tu.

⁵⁵ Vema, Yeye, Yeye alikuwa ni mtu mwema. Alikuwa Ndiye Mtu mwema wa pekee ambaye kweli tuliwahi kuwa Naye, ilikuwa ni Yeye. Ilibidi kuwapo na Mtu mmoja mwema apate kufa kwa ajili ya sisi watu wabaya, ku—kutufanya wema, sio kwa matendo yetu mema; kwa yale Mtu mmoja mwema aliyofanya, akakomboa kundi lote letu, mnaona.

⁵⁶ Na jinsi lingekuwa ni jambo la kijinga, baada ya njia moja tu ya ukombozi, na mpango mmoja tu kufanywa, kisha kuukataa huo. Hilo lingekuwa ni ja—jambo la kijinga kufanya, kuikataa njia ya pekee, mpango wa pekee; huyo ni Mungu, mpango wa Mungu. Ipo mipango mingine mingi; bali Mungu anao mpango, na huo mpango ni kupitia kwa Yesu Kristo, na Yeye pekee. Sio kupitia mfumo wowote, mfumo wowote wa elimu ama mfumo wowote wa kimadhehebu, wala chochote kile. Ni kupitia Yesu Kristo, na Yeye pekee. Huo ni mpango wa Milele wa Mungu, kupitia Yeye. Mungu daima hufanya mambo kwa njia moja. Kamwe habadilishi njia Yake ya kulifanya.

Sasa tunaona ya kwamba wengine husema, “Yeye alikuwa ni nabii.”

⁵⁷ Na, nabii, Yeye alikuwa, lakini alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa ni nabii, na zaidi. Na kulikuwako na manabii wengi. Manabii wote walikufia kwenye lango la mauti, bali Mtu huyu alichukua funguo, “mauti, kuzimu, kaburi,” kama Samsoni alivyoyafanya malango ya Gaza, akayachukua; akaondoa mwiba na mauti yenyewe, na kuyameza kwa ushindi, kisha akafufuka katika siku ya tatu, mshindi, anawafanya waaminio wake zaidi ya washindi. Imeshindwa tayari. Hakuna kitu kilichosalia ila kuingia moja kwa moja pamoja na wimbo wa washindi mioyoni mwetu. Yeye Ndiye Mshindi mkuu, na Huyu mkuu alikuwa ni zaidi ya nabii.

⁵⁸ Sasa, manabii walikuwa ni watu mashuhuri. Tu—tunajua hilo. Neno la Bwana liliwajia manabii; nalo huwajia, na hao pekee. Nasi tunaona ya kwamba hayo ni Maandiko, yale Hilo linayosema. “Yeye hatendi neno asipowaambia watumishi Wake, manabii, kwanza.” Nao walikuwa ni watu mashuhuri, lakini Mtu huyu alikuwa ni zaidi ya nabii.

⁵⁹ Sasa tunaona, basi, watu wengi wanadhani kwamba alikuwa mwanzilishi wa kanisa, inamfanya... alikuwa ni mtu mkuu mwenye akili nyingi, naye akaanzisha makanisa, alijua jinsi ya kuyaweka pamoja.

⁶⁰ Nilimsikia kasisi akizungumza, sio muda mrefu uliopita, kasema, “Yesu Kristo alilianzisha kanisa la kwanza la Kirumi, Naye anapaswa kujua jinsi ya kufanya hivyo.”

⁶¹ Sasa, Kanisa kamwe halikufanywa dhehebu, wala kamwe halikuanzia huko Rumi. Lilianzia Yerusalemu, kwenye Siku ya Pentekoste, wala sio Nikea, Rumi. Na Hilo... Wala Yesu hakuanzisha chochote. Yeye, jambo pekee alilofanya, lilikuwa ni kuita. Kamwe wewe, hujaundiwa dhehebu kwa Kristo; unazaliwa katika Ufalme wa Mungu.

⁶² Ndiyo—ndiyo kwanza nipite siku yangu ya kuzaliwa, Jumatatu iliyopita, nami nilikuwa na umri wa miaka hamsini na mitano. Nanyi mwajua, familia ya Branham kamwe haikuniomba nijiunge na familia hiyo. Nilizaliwa wa Branham.

⁶³ Na hivyo ndivyo tulivyo Wakristo. Tunazaliwa Mkristo, kwa nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. Nasi ni Wakristo kwa kuzaliwa. Hiyo, hiyo inatufanya viumbe vipya. Katika asili yetu ya kale, tusingeweza kuwa Wakristo. Hiyo ndiyo sababu, leo hii, tunao wengi sana wanaojiita Wakristo, na wanaishi maisha ya namna yoyote; kamwe hawajapata tu... hawajapata tukio la kule kuzaliwa mara ya pili, kile kitu Fulani kinachokubadilisha, kinachoondoa uhai huo. Kama vile kuivuta damu kutoka kwa mtu, na aliye na aina fulani ya damu, na kuitia ya aina nyingine ndani yake. Ni kuutoa uhai wa kale kutoka kwa mtu huyo, na kuingiza Uhai wa Kristo ndani ya mwaminio huyo, ndipo basi anakuwa kiumbe kipya. Yeye ni kiumbe kipya.

⁶⁴ Sasa njia pekee tutakayopata kujua, na tunayoweza kuwaridhisha watu wote... .

⁶⁵ Kama ningewauliza Wa—Wapentekoste, usiku wa leo, mnafikiri Yeye anapaswa kuwa ni nini? Wangemfanya “ni Mpentekoste.” Kama ningewauliza wa—wa Muungano wa Ndugu kile anachopaswa kuwa; “Mbona, Yeye alikuwa ni wa Muungano wa Ndugu.” Kama ningemwuliza Mmethodisti; “Mbona, Yeye alikuwa ni Mmethodisti.” Mbaptisti, na kadhalika.

⁶⁶ Lakini sasa kuna njia moja pekee ya ku—kuridhisha hilo, na kulifanya Kimaandiko. Sasa tunataka daima, kwenye jukwaa hili, kuwa sawa na Maandiko kabisa; kama sivyo, unawajibika kunijia na—na kunisahihisha. Sasa, inabidi iendane na Maandiko.

⁶⁷ Kwa hiyo njia pekee ya kujua kile Yeye alicholeo leo hii, ni kutafuta kujua kile alichokuwa. Mnaona? Hilo, Yeye alisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na kama tunaweza kujua kile alichokuwa, basi hana budi kuwa vivyo hivyo leo hii, kwa kuwa hawezi kubadilika. Biblia ilisema “Ni yeye yule,” y-e-y-e y-u-l-e, “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁶⁸ Sasa katika Yohana wa Kwanza, ama Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, tunaona. Haya hapa yale mwandishi aliyosema, kwa kutiwa pumzi na Roho Mtakatifu, yeye aliandika haya. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Huyo Neno alikuwa

pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.”

⁶⁹ Naweza kulichambua? “Hapo mwanzo alikuwa yule wa Milele.” Hata hakuwa ni Mungu. Mungu, neno letu la Kiingereza *mungu*, ni—ni “kitu cha kuabudiwa.” Lakini, Yeye, hapakuwapo na kitu chochote cha kumwabudu. Yeye alikuwa ni wa Milele tu.

⁷⁰ Ndani Yake mlikuwamo na sifa. Mtu yeyote anajua sifa ni nini. Kwa maneno mengine, ndani Yake mlikuwamo mawazo Yake, mawazo tu, hayo ni sifa Zake. Kisha, Neno Lake. Na wa—wazo, likitamkwa, ni Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno.” Kabla hata halijatamkwa, lilikuwa ni wazo, sifa.

⁷¹ Katika wazo hili, Yeye alikuwa awe ni Mungu. Labda aliwaumba Malaika, kwanza, kisha akaabudiwa. Alikuwa ni Mungu.

⁷² Halafu, basi, ndani Yake mlikuwamo na sifa kuwa Baba, kuwa Mwana, kuwa Mwokozi. Hakuna kilichokuwa kimepotea; ilibidi kitu fulani kipotee, kwa hiyo ilibidi pawe na njia iliyoandaliwa kwa ajili ya hicho. Kuwa Mponyaji; hakuna kigonjwa, kwa hiyo ilibidi afanye kitu fulani kiwe kigonjwa kusudi apate kukiponya. Inaonyesha tu sifa Zake.

⁷³ Na sasa, kumbukeni, kama uliwahi kuwa na Uzima wa Milele, ama utapata kuwa nao, ulikuwa nao pamoja Naye wakati huo. Unaona, ulikuwa Nao pamoja Naye. Kwa sababu, Yesu alikuja, na Yesu alikuwa ni Mkombozi. *Kukombo* chochote, ni, “kukirejesha” kutoka mahali kilipoangukia ama kilipotoka. *Kukikomboa*, “kukirejesha.” Nawe, jinsi unavyoonekana, kwamba wewe ni nani, nani, kwamba jina lako ni nani, hayo yalikuwa ni mawazo ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye Yesu alikuja sio kuokoa kitu hicho chote; Yeye alitaka kufanya hivyo, bali alikuja kukomboa, kuwarejesha hao waliokuwa kwenye mawazo Yake kabla ya mwanzo.

⁷⁴ Hiyo ndiyo sababu, Yeye alikuwa Neno lililofanyika mwili. Mnaona? “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Neno, mawazo ya Mungu ya jinsi angelifanya, Yeye alijidhihirisha katika Yesu Kristo. Ilikuwa ni Mungu akifanyika mwili.

⁷⁵ Sasa, mahali ulipo sasa, huna budi kufa, kwa kuwa wewe bado. . . Ni kama tu kupiga picha. Wewe ni negativu. Negativu yoyote haina budi kuingizwa kwenye chumba cha kusafishia picha, kwa asidi, kuisafisha picha, kukufanya uone jinsi ilivyo. Sisi sasa tuko katika mfano Wake uliodhihirishwa. Ni negativu iliyochukuliwa, sisi ni uhai wa kibinadamu. Lakini inatupasa tuingie kwenye chumba cha kusafishia picha, chini kaburini, tupate kupitia kusafishwa, turudi katika ile sura; loo, jamani, tukiwa wachanga milele, uzee wote na ninii yote. . . dosari na kila kitu kitaondolewa.

⁷⁶ Kisha tunakombolewa, sifa za Mungu, kurejeshwa moja kwa moja. Mungu, mwili, pamoja na Kristo ndani ya Kanisa; kama tu vile mume na mke wake, hiyo ni kweli, Kristo na Bibi-arusi. Maana, inayakomboa tena, mawazo Yake, nayo mawazo Yake yanadhihirishwa.

⁷⁷ Sasa unasema, “Hiyo ilichukua muda mrefu sana.” Sio kwa Mungu. Sisi ni wenye kikomo. Hatuna budi tu kuharakisha.

⁷⁸ Nilikuwa nikiwazia. Nilipoondoka Jeffersonville, na kuendesha maili thelathini kwa saa, niliendesha motokaa kwenda Birmingham katika siku moja na sehemu kidogo ya usiku, nami nikawazia hilo halikumaanisha mengi sana kwangu. Lakini vipi kama maskini siafu mdogo alijaribu kufika huko? Jinsi hilo lingamaanisha kwake! Mnaona, asingeweza kufika katika maelfu ya muda wa maisha. Lakini halikumaanisha kitu kwangu, sio mengi kwangu. Na ndege je? Na jeti? Halafu, na mwanaanga je? Kisha, na Mungu je?

⁷⁹ Mnaona, Yesu alisulubishwa tu jana jioni, katika wakati wa Mungu, kama angalikuwa na wakati. “Miaka elfu moja ni siku moja tu kwa Mungu, tuseme.” Hata sivyo. Ni kwamba, “ni kama ilikuwa, siku moja.” Kwa hiyo huu haujafikia hata juma moja, endapo unataka kumhesabia wakati, huo wote tangu mwanzo wa uumbaji, tukiufafanua tu.

⁸⁰ Mungu pamoja na mawazo Yake, akifanyika mwili, kisha hiyo inatuletea Uzima wa Milele. Nao Uzima wa Milele, kuna aina moja tu Yake, hiyo ni Mungu. Halafu ni Mungu akidhihirishwa katika Kanisa Lake, kama vile Mungu alivyodhihirishwa katika Mwanawe. Ni Mungu yeye yule wakati wote. Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; Mungu ndani yetu; kurudisha tu kitu hicho chote moja kwa moja tena.

Sasa, “Hapo mwanzo alikuwako Neno.”

⁸¹ Sasa kama tulikuwa tukitaka kuzungumza kuhusu ni nani atakayehukumu ulimwengu, mbona, ungeninii, mtu fulani angesema... Nilimsikia Mkatoliki, kasema, “Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa Katoliki.” Kama akifanya hivyo, ni kanisa Katoliki lipi? Mnaona, wana mengi mbalimbali ya hilo. La Orthodoxi, la Kiyunani, ama la Kirumi, ama kitu gani, mnaona, atauhukumu ulimwengu kwa kanisa Katoliki ipi? Vema, kama akiuhukumu kwa kanisa la Katoliki, basi la Kiporotestanti liko nje. Kama akiuhukumu kwa kanisa la Kiprotestanti, basi la Katoliki liko nje. Kama akiuhukumu kwa Methodisti, la Kibaptisti liko nje. Vema, unasema, “Ngoja kidogo, yote ni...” Loo, la.

⁸² Kumbukeni, hapo mwanzo, lile, lile la pekee lililoimarishwa, lile la... ambalo Mungu aliwapa Adamu na Hawa, lilikuwa ni kukaa nyuma ya Neno Lake. Na sio tu kuninii... Shetani hakukosa kulia-... hakumwambia halikuwa hivyo. Yeye alinukuu vibaya tu fungu dogo Lake. Na kama maskini fungu

moja dogo lilisababisha shida hizi zote, magonjwa, na huzuni kubwa, na majonzi, fungu moja dogo litatutenga Nalo.

⁸³ Mungu atauhukumu ulimwengu sio kwa kundi fulani. Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, Naye Kristo ni Neno. Yeye ni Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Huyo Neno alikuwako pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Kwa hiyo Yeye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa katika kila wakati. Anamfanya yeye yule jana, leo na hata milele.

⁸⁴ Alijitambulisha Mwenyewe, hapo mwanzo, pamoja na manabii. Sasa, kumbukeni, manabii ndio Bwana anaonena kuwapitia. Pia—pia sasa angalia, Yeye alijitambulisha Mwenyewe katika wanadamu, tangu mwanzo kabisa, tangu mwanzo kabisa wa wakati.

⁸⁵ Yeye daima anayo njia ya kufanya mambo, na Yeye kamwe habadilishi njia Yake. Hiyo ndiyo sababu ninaweza kuliadini Neno Lake. Kama Mungu alipata kuitwa jukwaani kufanya tendo; nao uamuzi alioitoa Mungu wakati alipoitwa jukwaani, Yeye hana budi kutenda vile vile kila wakati anapoitwa jukwaani, la sivyo alifanya kosa mara ya kwanza. Vinginevyo, kama alitwa kumwoko mwanadamu, Yeye alimwoko kwa msingi fulani; basi kama akiitwa kumwoko mwanadamu mwingine, hana budi kufanya sawa na alivyofanya mara ya kwanza, la sivyo alikosea wakati alipolifanya kwa njia ya kwanza. Kama akipata kuitwa jukwaani kumponya mtu, Naye akamponya katika misingi ya jambo fulani; kama akipata kuitwa tena kuponya, hana budi kuponya kwa misingi ile ile, la sivyo alikosea. Naye hana kikomo, anaenea kila mahali, ni mjua yote. Yeye—Yeye ni Mungu asiye na kikomo, kwa hiyo habadiliki.

⁸⁶ Sasa, sisi tuna kikomo. Tunaweza kusema *hii* ni kweli, leo hii, kesho tunaweza kupata kitu kingine. Tunaweza kuwa bora. Tunakuwa bora, tunajenga nyumba bora kuliko tulizojenga miaka mia moja iliyopita. Tuna magari bora kuliko tuliyokuwa nayo miaka ishirini iliyopita, na tuna usafirishaji bora, na chochote zaidi unachotaka kukiendea. Sisi ni bora kwa kuwa tunajifunza.

⁸⁷ Lakini Mungu hajifunzi, kwa kuwa Yeye ni mkamilifu, kwanza kabisa. Kwa hiyo, Yeye na Neno Lake ni mmoja, kwa hiyo Neno Lake ni kamilifu. Kama huamini hilo, kamwe usingie kwenye mstari wa maombi, maana huo ndio msingi pekee unaoweza kukubali chochote. Imani inaweza tu kutulia juu ya kitu ambacho ina hakika nacho, na imani halisi kabisa hutulia tu kwenye Mwamba wa Milele wa Neno la Milele la Mungu. Hausogei. Unadumu tu pale pale, haidhuru. Nena kuhusu ule mwamba wa Gibraltari? Hapo inaposimama ni juu ya Mwamba wa Nyakati. Neno kamwe haliwezi kubadilika, nayo imani inatulia juu ya Hilo. Kasema, “Mbingu na nchi zitapita, bali

Maneno Yangu hayatahindwa kamwe.” Wanaume na wanawake waliopata kuwa chochote, walikuwa ni wanaume na wanawake walioamini hilo kuwa ni Kweli. Na hiyo ni Kweli. Yeye, Neno, ni Kweli.

⁸⁸ Sasa tunaona ya kwamba Yeye, hapo mwanzo, Mungu alitenga Neno kiasi fulani kwa kila wakati, kwa kila—kila wakati. Ndipo basi wakati unapofikia kwa Neno hilo kufunuliwa... Msikose hili. Wakati unapofikia kwa Neno hilo kufunuliwa, kwa kawaida mwanadamu alilivuruga sana, mpaka Yeye akamtokea nabii. Yachunguzeni Maandiko. Mnaona? Sasa kumbukeni, Mungu asiyebadilika, Yeye hawezi kubadilisha njia Zake. Hana budi kulifanya vivyo hivyo kila wakati, pasipo kubadilika.

⁸⁹ Hebu niwapeni tu mfano mmoja. Wakati mwanadamu alipoanguka, akatenda dhambi, basi Mungu aliitwa, ama amtupilie hukumuni au amfanyie njia ya kuepukia. Sasa, Mungu, katika bustani ya Edeni, alifanya mpango mmoja wa kumwokoza mwanadamu, njia moja, na hiyo ilikuwa ni kupitia kwa Damu iliyomwagika ya mhusika asiye na hatia. Kamwe hajaibadilisha. Tumejaribu kujenga miji, minara, kuelimisha, kuunda madhehebu, bali yote yameshindwa. Mungu anaweza tu kukutana na mwanadamu chini ya Damu iliyomwagwa ya Asiye na Hatia. Alifanya hivyo katika bustani ya Edeni, wala kamwe hajaibadilisha.

⁹⁰ Wala Mungu kamwe habadilishi njia Zake. Yeye, kama akizibadilisha, basi Yeye ana kikomo kama nilivyo mimi, ulivyo wewe. Tunasema, “Vema, nilikosea *hapo*, bali ni—nitakuwa sahihi wakati huu.” Sio Mungu. Yeye ni sahihi mara ya kwanza. Haimbidi kubadilisha chochote. Alifanya ahadi, Naye ni Mungu, anadumu nayo.

⁹¹ Kama vile Ibrahimu, alishawishika ya kwamba Mungu aliweza kutimiza lolote aliloahidi, kwa hiyo akaita chochote kinyume na hilo Neno kana kwamba hakikuwako. Yeye aliendelea tu vivyo hivyo moja kwa moja, dhidi ya ninii ya kisayansi, mathibitisho ya kisayansi, na dhidi ya hoja, dhidi ya tumaini, dhidi ya kila kitu kilichokuwapo. Neno la Mungu lilikuja kwanza. Ibrahimu alisema, “Kitu kingine chochote na kiwe makosa.” Alikuwa atampata mtoto, haidhuru. Na kwa hiyo akampata, mnaona, kwa sababu aliliamini.

⁹² Sasa tunaona, basi, ya kwamba Mungu asiyebadilika daima hufanya vile vile. Sasa angalia, kwa kifupi tu, katika historia ya wakati. Ambatana na mimi sasa, kwa dakika chache tu zifuatazo. Hebu turudi nyuma tuone.

⁹³ Hapo mwanzo Yeye alisema na manabii, nalo Neno la Bwana lilimjia nabii. Naye nabii, akiwa anaweza kutabiri, mambo ya kiungu, nayo yakatukia tu jinsi hiyo, ulikuwa ndio utambulisho wake. Nabii, *mwonaji*, linamaanisha, “mtu

anayetabiri ama anayenena kimbele,” na pia ni “mfasiri wa Kiungu wa Neno lililoandikwa.” Mtu yeyote anajua hilo, anayejua maana ya nabii.

⁹⁴ Sasa Neno la Kiingereza, *nabii*, n-a-b-i-i, linamaanisha, “mhubiri,” mtu yeyote tu anayehubiri.

⁹⁵ Lakini mwonaji katika Agano la Kale, ambaye alitajwa kama nabii, yeye ndiye aliyeyaona mambo kimbele. Yeye alisema, “Kukiweko na mtu miongoni mweni aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha kwake. Na yale asemayo yakitimia, basi msikieni; bali yasipotimia, msimsikilize nabii huyo, mnaona, maana anatabiri uongo. Bali ikiwa nimemtuma, huo utakuwa ndio utambulisho Wangu, asemayo yatatimia. Yeye amezaliwa ulimwenguni, akawekwa wakfu, akachaguliwa tangu zamani na Mungu kufanya hivyo.” Maana, “Karama zote na miito hazina majuto.” Zimechaguliwa tangu zamani na Mungu.

⁹⁶ Kabla ulimwengu haujaanza kamwe, Yeye alijua yote kuuhusu. Alijua kila kiroboto, kila nzi, na kwamba atatoa shahamu kiasi gani, na ni mara ngapi angeyapepesa macho yake. Hiyo—hiyo ni kutokuwa na kikomo, mnaona, kutokuwa na kikomo. Hiyo ni ninii tu... Kama sivyo, basi Yeye si asiye na kikomo. Alijua kila kitu. Naye ni... Yeye ni mjua na mjua yote. Kwa kuwa anaenea kote, hiyo inamfanya... Kujua yote kunamfanya mwenye kuenea kote. Anajua kila kitu, alikijua kabla ulimwengu haujaanza.

⁹⁷ Yeye alijua, kabla ulimwengu haujaanza, tungeketi hapa. Alijua ni mara ngapi ningeinua mkono wangu juu chini. Sasa Yeye alijua maneno ambayo ningesema. Alijua ni mara ngapi ungeyapepesa macho yako, kile ungewazia, kabla ulimwengu haujaanza kamwe. Tunaogopa nini? Mungu ni Baba yetu. Hiyo ni kweli. Yeye ni Baba yetu. Hatuna wasiwasi. Watu wamepoteza tu imani yao na matumaini Kwake.

⁹⁸ Nasi tunaona ya kwamba hilo linaenda kwa majira, halafu kuna Maneno ambayo Mungu ameyanena yapate kutimia. Halafu wote watakuwa wakichanganyikiwa; ndipo Mungu anatutumia nabii jukwaani, ndipo basi nabii huyo analithibitisha Neno hilo kwa ajili ya wakati huo, daima. Pitia kwenye Nyakati za Kanisa, zile tunazopaswa kuwa nazo, uone kama hutawaona hao watu kote katika Nyakati za Kanisa kama tunavyowaona, tangu wa—wale mitume. Sasa angalieni hili, tena.

⁹⁹ Mungu alinena na Nuhu, naye alikuwa ni nabii, akamwambia yale yanayokuja. Alitabiri, nayo yakatukia.

¹⁰⁰ Sasa moja kwa moja akaja Yusufu. Yusufu, mfano mkamilifu, huyo alikuwa ni Kristo katika Yusufu. Mbona, mnaona, alipendwa na baba yake, akadharauliwa na ndugu zake, kwa kuwa alikuwa ni mwonaji. Walimchukia, pasipo

sababu. Mtu huyo asingejisaidia, kile alichokuwa alikuwa. Nao hao ndugu wengine walimchukia, mfano mzuri sana wa nyakati zote. Daima, wakati mwonaji anapojitokeza jukwaani, hao wengine humchukia, kwa sababu ile ile waliyomchukia Yusufu. Asingeweza kujisaidia. Alininii. . . Angeweza kufasiri ndoto zao; kamwe hakukosea. A—alitabiri mambo; kamwe hakukosea. Nao ndugu zake wakamchukia, pasipo sababu.

¹⁰¹ Pia, angalieni, maisha yake yalimwonyesha Kristo kwetu, kikamilifu. Hata aliuzwa, kwa karibu vipande thelathini vya fedha, akatolewa kwenye handaki; akawekwa kwenye mkono wa kuume wa Farao, mtawala wa ulimwengu siku hiyo. Na kila mara alipoondoka kwenye nyumba ya mfalme, walipiga parapanda, na kusema, “Kila goti lipigwe, maana Yusufu anakuja.” Mfano mkamilifu wa Kristo katika ule Utawala wa Miaka Elfu; hapo parapanda itakapolia na ninii. . . Yeye atajitokeza, na kila goti litapigwa na kila ulimi utamkiri.

¹⁰² Angalieni, katika gereza lake, yeye alikuwa ni nabii. Huo ni wakati alipouzwa na kuwekwa gerezani, kwa sababu ya mke wa Potifa. Ndipo tunaona ya kwamba mle ndani mchinja nyama na mwokaji, wote wawili waliota ndoto, naye akaifasiri ndoto hiyo, kisha mmoja akapotea na huyo mwingine akaokolewa. Vivyo hivyo na Yesu msalabani, kabisa; mmoja alipotea, mmoja akaokolewa, wakati alipokuwa gerezani Mwake, ametundikwa Msalabani. Ni mfano mkamilifu tu.

¹⁰³ Tunaona ya kwamba wakati Musa alipojitokeza jukwaani sasa, sasa, Musa asingekuwa katika Roho yeye yule wala kwa njia ile ile, pamoja na ujumbe ule ule a—aliokuwa nao Nuhu. Ilikuwa ni wakati mwingine, kulitimiza neno lingine. Mungu alisema, “Uzao wako utakuwa mgeni katika nchi ya ugeni, u—uwe mtumishi kwa muda wa miaka mia nne, ndipo nitawatoa kwa mkono wenye nguvu.” Lakini Musa wakati alipoitwa; ilimchukua miaka arobaini ya mafunzo, kisha miaka arobaini ya kuyaondoa kwake tena, ndipo Mungu akamwita kwa Nuru ya kimbinguni, Nguzo ya Moto ikiwa kule nyuma kwenye kichaka kilichowaka moto. Naye alijua zaidi kumhusu Mungu, katika dakika tano, kuliko alivyosoma kwa muda wa miaka arobaini, kwa kuwa alikuwa katika Uwepo Wake. Hilo ndilo mimi. . .

¹⁰⁴ Wakati mtu anapokuwa katika Uwepo wa Mungu, basi anajua jambo fulani. Anajua jambo fulani.

¹⁰⁵ Sio, hawezi kujifunza hayo katika vitabu. Huwezi kumjua Mungu kwa vitabu. Elimu inachukua. . . Unasema, “Yeye ni D.D.D., Ph.D.” Hiyo inampeleka tu mbali zaidi kutoka kwa Mungu, kwangu mimi. Humjui Mungu kwa elimu.

¹⁰⁶ Unamjua Mungu kwa imani, nawe unamwamini. Hivyo ndivyo unavyomjua Mungu. Na, hata hivyo, hiyo ndiyo sababu ninafikiri mikutano yetu, katika Uwepo wa Kiungu wa Mungu, inapaswa kuichochea imani ya watu kujua hivyo; haidhuru

sayansi inasema nini, yale asiyeamini anasema. Kristo alitumwa kwenu, waaminio. Mna haki ya kuufurahia ushirika Wake na baraka Zake, na kila kitu alichofia. Haya basi.

¹⁰⁷ Hakuna mtu aliye na haki ya kuihubiri Injili mpaka amepiga magoti kwenye changarawe hizo takatifu huko nyuma Mbele ya hiyo Nguzo ya Moto, na kuisikia Sauti ya Mungu ikinena naye. Mwajua, dini siku hizi zinaweza kulielezea lote vinginevyo, “Na *hili* lilitukia, na Lile limepita. Nalo Hili lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine, na *hili*.” Bali mtu aliyewahi kukutana na Mungu, uso kwa uso, na kuzungumza na Yeye, hakuna mwanasayansi wala pepo yeyote, wala chochote kingine, kinachoweza kuja mahali hapo patakatifu. Yeye alikuwa hapo ambapo alikutana na Mungu, naye anajua kile anachozungumzia, na hakuna haja ya mtu mwingine yeyote kujaribu kumwambia.

¹⁰⁸ Mungu akinena katika hizo nyakati, kupitia manabii Wake, akijitambulisha Mwenyewe kila wakati kupitia wakati unaokuja.

¹⁰⁹ Sasa moja kwa moja alikuja Yesu wa Nazareti. Yeye alikuwa ni nabii, pia. Biblia ilisema angekuja. Kumbukumbu la Torati 18:15, Musa alisema, “Bwana Mungu wako atawainulia nabii aliye kama mimi, nao watu watamsikiliza.”

¹¹⁰ Sasa angalia kila wakati, Israeli yote, watu wote waliamini hilo, hao manabii, wakati wakiwa ni manabii waliotambulishwa. Waebrania thela-. . . Waebrania mlango wa kwanza, ilisema, “Mungu zamani za kale na kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu kwa njia ya manabii; katika siku hizi za mwisho, kupitia Mwanawe Yesu Kristo.” Mnaona, kupitia Mwanawe Yesu Kristo. Angalieni, kamwe habadilishi njia Yake; jambo lile lile, daima ni mfululizo wa Neno la Mungu. Mungu kamwe hakutumia mfumo fulani, kamwe hakutumia dhehebu, kamwe hakutumia makundi. Yeye humtumia mtu mmoja binafsi.

¹¹¹ Kama wewe ni Methodisti, Baptisti, hiyo ni sawa; Presbiteri, Pentekoste, hilo ni sawa; lakini Mungu anakushughulikia kama mtu binafsi. Ni wewe, sio kanisa lako. Wewe ndiwe unayewajibika, si yale kanisa lako lisemayo. Yale Mungu aliyokuambia! Hayana budi kulingana na Neno. Naam, Mungu hushughulikia watu binafsi. Daima amefanya hivyo.

¹¹² Manabii, hakuna shule ya manabii. Walijaribu hiyo wakati mmoja wakashindwa. Kwa hiyo waliona, Ahabu alikuwa na kundi lao huko chini. Lakini Mungu alikuwa na mmoja, pia, jina lake Mikaya, ambaye hao wengine wote walimchukia, lakini alikuwa na ile Kweli wakati huo, alikuwa na kweli ya Neno, kwa sababu unabii wake ulikuwa ni kulingana na Neno.

¹¹³ Haina budi kuwa hivyo daima. Nabii hutumwa kulithibitisha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo.

114 Sasa hivyo ndivyo hasa walivyoshindwa kumwona Yesu. Hivyo ndivyo hasa. Waangalie watu hao, hao Mafarisayo na Masadukayo, wasomi tusio nao siku hizi. Hawana budi kuzaliwa ninii, kutoka kwa kabila fulani, Lawi. Babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu zao walikuwa ni makuhani, kote kote. Walijifunza Neno hilo, mchana na usiku, mchana na usiku. Lakini Neno hilo lilipothibitishwa, hawakulijua. Mnaona, walikuwa na mapokeo. Yesu alisema, “Ninyi kwa mapokeo yenu mmelitangua Neno la Mungu.” Sasa, Yeye alikuja vile hasa nabii alisema angekuja, bali, mnaona, walikuwa na mapokeo wala wasingeweza kuliona Hilo.

115 “Huyu mtoto mchanga aliyezaliwa huko chini, aliyezaliwa haramu, na katika hori la ng’ombe, hiyo ingewezekanaje? Pia jamaa huyu hakwenda kwenye shule yoyote. Hakuwa na vitambulisho vyovyote. Hakuwa na kadi ya ushirika. Hakuwa mfuasi wa shirika lolote. Hawakujua shule aliyohudhuria. Huyu angewezaje kuwa chochote?” Lakini ilikuwa. Walishindwa kuona.

116 Alisema, “Kazi nizifanyazo, zinanishuhudia Mimi. Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yao mnadhani mna Uzima wa Milele; Nayo Ndiyo yanayoshuhudia, kuwaambia kwamba Mimi ni Nani. Hayo Ndiyo ushuhuda Wangu, Maandiko.” Kasema, “Msiponiamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo. Zinawaambia kwamba Mimi ni Nani.”

Wakasema, “Tunaye Musa. Tunamwamini Musa.”

117 Kasema, “Kama mlimwamini Musa, mngeniamini Mimi; aliandika habari Zangu.” Mnaona?

118 Walikuwa na giza sana, hata hivyo wasingeweza kuliona. Unashangaa kama hilo lisingeweza kujirudia? Limetabiriwa kujirudia, mwajua. Lilitabiriwa hivyo, pale.

Mnasema, “Katika siku hii?” Loo, naam.

119 “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiofanya suluhu, wasingizaji, wasiojizua, wasiopenda walio wema, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao mjiepushe nao.” Imetabiriwa, na unabii wote hauna budi kutimizwa. Sijui kama tuko karibu na wakati huo. Sijui kama tumeukaribia. Hebu tuangalie huku na huku kidogo tu tuone jinsi tulivyo na faraja Zayuni. Sasa tunaona.

120 Hebu tuone kile Yesu alichokuwa, hapo alipokuja. Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ni Neno kabisa. Nalo Neno daima husahihisha. Hulisahihisha kosa. Ingawa kosa haliliamini, wakati mwingine, bali Neno husahihisha kosa.

121 Mwangalie Yesu, kwenye umri wa miaka kumi na miwili tu; mvulana mdogo kama jamaa huyu aliyeketi hapa amelala usingizi, mwenye magango miguuni mwake. Yesu alikuwa

m—mvulana mdogo, yapata umri wa miaka kumi na miwili; hamna kumbukumbu ambapo alipata kwenda shuleni. Lakini walipanda kwenda kwenye Karamu ya Pasaka, na wakati wao...ama kwenye Karamu ya Pentekoste, hasa. Nao wakapanda kwenye karamu, Yusufu na Mariamu, na kusanyiko lote kutoka huko mjini. Wakaenda Yerusalemu. Na safari ya siku tatu, wao wakidhania Yeye alikuwa hapo karibu pamoja na watu na baadhi ya jamaa zao kule. Lakini wakamkosa. Wakaenda kumtafuta, wala hakuwako. Wakarudi Yerusalemu wakamkuta hekaluni, akibishana na makuhani, akibishana na hao watu.

¹²² Angalieni hapa, sio kuwaudhi ninyi Wakatoliki. Lakini ninyi mnaomchukua Mariamu kama mungu mke ama mwombezi, angalieni hapa. Yeye alitoa ushuhuda, angalieni aki hukumu ushuhuda wake mwenyewe. Alisema, “Mimi pamoja na baba yako tumekutafuta, kwa machozi.” Angalieni kile alichofanya. Ali hukumu ushuhuda wake mwenyewe. Alikuwa akimwita Yusufu baba Yake.

¹²³ Lakini angalia. Mtoto tu, mvulana mdogo tu, bali Neno daima hulisahihisha kosa. Kasema, “Hamjui kwamba inanipasa kuwa kwenye shughuli za Baba Yangu?” Neno lenyewe, mnaona, lilisahihisha hilo kosa.

¹²⁴ Akasema, “Mimi na baba yako,” Yusufu. Papo hapo mbele ya hao makuhani, ambao alikuwa tayari amewaambia alipata mimba kwa Roho Mtakatifu, na hapa alikuwa ameshuhudia na kumtambulisha Yusufu kama baba Yake, aki hukumu ushuhuda wake mwenyewe.

¹²⁵ Lakini angalieni Neno likilibaini. Yeye alikuwa ni Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa ni Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Neno lililibaini, kulisahihisha hilo kosa.

¹²⁶ “Hamjui inanipasa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?” Kama Yusufu angalikuwa ni baba Yake, angalikuwa huko chini katika duka la seremala, katika shughuli zake. Bali shughuli za Baba Yake zilikuwa ni kuyahukumu hayo madhehebu na kadhalika, Naye alikuwa akiyahukumu huko juu, ambako Yeye—ambako ndio Kwake. Alikuwa na wa—wakati mzuri kule, ambako hao hata wasingefahamu jinsi ambavyo mvulana huyu angejua mambo kama hayo. Lakini Yeye alikuwa ni Neno. Hakuna mtu aliyepata kunena kama Yeye. Yale aliyosema, alikuwa na mamlaka ya kuyafanikisha.

Hao manabii walikuwa nayo, pia, maana waliishi kwenye wakati huo.

¹²⁷ Yeye alikuwa, Yeye—Yeye alikuwa manabii wote wakiunganishwa katika Mmoja, pamoja hata na huyo, maana Yeye alikuwa ni utimilifu wa Neno. Alikuwa ni Neno lote.

Manabii walikuwa ni Neno tu la wakati huo, bali Yeye alikuwa ni Neno kwa nyakati zote. Alikuwa ni Mungu, Mwenyewe, akishuka na kujidhihirisha katika mwili wa nyama. “Neno aliyefanyika mwili akakaa miongoni mwetu.”

¹²⁸ Hebu tuone jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe, mara Yake ya kwanza, baada ya kutoka nyikani, kutoka kwenye kubatizwa na Roho Mtakatifu. Kubatizwa, na Yohana. . . Hili hapa wazo dogo ambalo mnaweza kulishika kabla tu hamjaliwazia.

¹²⁹ Je! mnajua Biblia inasema, “Neno humjia nabii”? Kukiweko na nabii nchini, Neno halina budi kumjia.

¹³⁰ Hebu mwangalieni Yohana, alikuwa ni nabii, wa kwanza waliyekuwa naye, mnaona, naye alikuwa ni nabii Neno. Na wakati alipokuwa amesimama pale, akitabiri, Neno lilimjia majini. Yesu alikuwa ni Neno, akaingia moja kwa moja ndani ya maji. Ndipo Yohana akasema, “Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe. Mbona Wewe waja kwangu?”

¹³¹ Naye akasema, “Kubali iwe hivi, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote.” Kwa nini? Basi Yohana akiwa ni nabii, Naye akiwa ni Neno, alijua Yeye alikuwa ni Dhabihu, kwa hiyo Dhabihu haina budi kusafishwa kabla haijatolewa. Kwa hiyo akambatiza Yesu, akiliosha Neno, kabla halijatolewa, mnaona. Kwa hiyo akamba-. . . Akasema, “Kubali iwe hivi sasa, kwa kuwa imetupasa kuitimiza haki yote.”

¹³² Basi alipomruhusu, Yesu alitoka moja kwa moja majini. Na, tazama, mbingu zikafunguka, naye akaona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka juu Yake. Ndipo akaenda nyikani, akajaribiwa kwa muda wa siku arobaini, kisha akatoka.

¹³³ Hebu tuifuatilieni huduma Yake sasa. Tuko katika Yohana Mtakatifu 1. Hebu tuone kinachotukia, na tuone kile alichokuwa wakati huo, ndipo tunaweza kuona kile alichokuwa sasa, basi. Hebu mwangalieni kwenye nyakati zilizopita, sasa, tuko kwenye wakati wa Yesu.

¹³⁴ Ndipo tutafunga, labda tulichukue kesho usiku, pale. Tuna dakika chache tu zilizosalia.

¹³⁵ Huyu hapa anakuja, kutoka nyikani. Jambo la kwanza, kulikuwako na mtu jina lake A—Andrea. Alikuwa akienda kuhudhuria ujumbe wa Yohana. Ndipo Yohana akaanza kusema. . . .

¹³⁶ Yohana alijua ya kwamba alikuwa a—awe ndiye mtambulishi wa Masihi, kwa kuwa tayari alikuwa amesema, mwajua. Baba ya—yake alikuwa kuhani, bali kamwe hakumfuata baba yake. Kazi yake ilikuwa ni muhimu sana asingeweza kwenda kwenye yoyote ya shule hizo za kithiolojia, kwa hiyo akaenda nyikani kwenye umri wa miaka tisa. Alijua ilimbidi kumtambulisha, ilimbidi kuona ishara ambayo ingethibitisha kwamba huyo—huyo Masihi alikuwa ni nani. Naye alilijua kwa udhahiri kabisa,

alijua wito wake, alikuwa na hakika sana nao, hata alipokuwa amesimama kati ya kundi kama hili la watu, akasema, “Yeye yumo miongoni mwenu sasa. Kuna Mtu amesimama miongoni mwenu, msiyemjua. Atabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.” Kasema, “Sistahili hata kuvifungua viatu vyake.”

¹³⁷ Halafu basi, jambo la kwanza, Yesu akatoka moja kwa moja, naye akaiona ishara hiyo. Akasema, “Niliiona ishara, nami nina hakika kwamba huyo alikuwa ni Yeye.” Basi akambatiza. Sasa wakati Yesu. . .

¹³⁸ Na hapana shaka kwamba Andrea alikuwa amemwambia ndugu yake. Sasa, ndugu yake kwa namna fulani alikuwa. . . Simoni, kidogo alikuwa mmoja wa jamaa hawa wagumu ambao hawakutaka kuamini chochote. Akasema, “Nakumbuka yale baba yangu aliyoniambia, alisema, ‘Mwanangu,’ siku moja alisema, ‘unajua, tumevua samaki, nasi tumemtumainia Mungu ku—kutupa samaki, tupate kulipa madeni yetu na kupata chakula.’ Akasema, ‘Mara nyingi imetubidi kuomba, zamani sana kabla mama hajafa na kadhalika, kutupa mavuno mazuri ya samaki, tupate chakula cha siku hiyo. Nami daima nimekutazamia, kama impasavyo Mwebrania yeyote mzuri, kule kuja kwa Masihi.’ Kasema, ‘Sasa ninazeeka, nami nadhani sitamwona. Lakini nawatakeni ninyi wavulana mjue, kabla tu ya Yeye kujitokeza jukwaani, kutakuwako na kila namna ya mambo ya uongo yatakayoibuka, mnaona, bali ninawatakeni mjue, hatuna budi kuliadini Neno. Musa nabii wetu alitwambia, ya kwamba, “Bwana Mungu atamwondokeshwa nabii.” Sasa hatujakuwa na nabii kwa mamia na mamia ya miaka. Bali Masihi atakapokuja, atakuwa ni nabii aliyetambulishwa. Sasa, mtamjua, maana atakuwa ni nabii.”

¹³⁹ Halafu jamaa huyu alikuwa akihubiri, hafanyi kitu kingine ila kuhubiri, Yohana. Kwa hiyo yeye, Simoni, asingeweza kumfuata huyo.

¹⁴⁰ Kwa hiyo akamwambia ya kwamba Huyu aliyekuwa akinena habari zake alikuwa amekuja, kwa hiyo hilo lilimtambulisha kama nabii, mnaona, kwamba Yeye. . . kile kilichofanyika, jinsi kilivyotukia.

¹⁴¹ Kwa hiyo Andrea na Simoni wakashuka wakaenda siku moja, na kuzisafisha nyavu zao, nao wakashuka wakaenda kumwona Yesu. Ndipo Simoni alipokuja, akaenda mbio katika Uwepo Wake, Yesu alimwangalia na kusema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Hilo lilitosha. Alijua papo hapo kwamba huyo alikuwa ni yule Neno aliyefanyika mwili. Mnaona, Yeye alilijua.

¹⁴² Kwa nini? Waebrania mlango wa 4, kifungu cha 12, ambacho kinajulikana na wasomi wote, kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Ni wasomaji wangapi wanaojua hilo?

[Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kweli. Waebrania 4, hiyo ni kweli, 4:12.

¹⁴³ Sasa, wakati alipoona hilo, alijua ya kwamba Yeye hakujuu tu kwamba alikuwa ni nani, alimjua yule baba yake mzee mtauwa, pia. Alijua papo hapo huyo alikuwa ni Masihi. Akapewa funguo za Ufalme, baadaye.

¹⁴⁴ Halafu kulikuwako na jamaa fulani aliyekuwa amesimama pale, jina lake Filipo. Kwa hiyo alikuwa na jamaa aliyekuwa akisoma Biblia pamoja naye, loo, kwa miaka mingi, na huyo alikuwa ni jamaa mmoja jina lake Nathanaeli. Aliishi yapata maili kumi na tano, kama ukiangalia kwenye ramani, mahali alipokwenda, kukizunguka kilima kumtafuta Nathanaeli. Basi alipompata... Yeye alikuwa—alikuwa ni mtu wa msituni. Alikuza mizeituni, naye alikuwa huko msituni, akiomba. Na, hakika, Nathanaeli, baada... ama Filipo, samahani. Filipo, baada ya kumwona Nathanaeli akiomba, yeye alikuwa ni muungwana, alingoja mpaka akamaliza kuomba. Yeye, wakati aliposimama, alisema, “Aisee! Njoo, mwone Yeye tuliye mpata! Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu, huyu ni—huyu Ndiye Masihi tunayenena habari zake.”

¹⁴⁵ “Loo!” Basi msikilize jamaa huyu. Kasema, “Sasa, laweza neno jema kutoka kwenye kundi la watu kama hao, kutoka kwao?”

¹⁴⁶ Nami nafikiri yeye alimpa jibu zuri sana mtu yeyote angaliweza. Kasema, “Njoo uone.”

¹⁴⁷ Usi—usikae nyumbani na kukosoa. Njoo ujionee mwenyewe. Kuja pamoja na Neno lako, na hebu tulichunguze tuone ni nini. Unajua kile Neno linachosema Masihi huyu atakuwa. Kile alichokuwa jana, ndicho alichio leo. Lichunguze Neno, uone Yeye ni nini. Kama Yeye ni shirika, kama Yeye ni kundi la watu, Yeye ni kitu gani? Mnaona?

¹⁴⁸ Kwa hiyo tunaona hapo kwamba wamekizunguka kilima, na hapana shaka kwamba Filipo alimwelezea kile alichokuwa amesema. “Vema, maskini mzee huyo mvuvi asiyekuwa na elimu ya kutosha kutia sahihi risiti, hiyo ni wakati aliponunua samaki, Yeye alimwambia kwamba yeye ni nani na kumwambia baba yake alikuwa ni nani. Haitanishangaza kama Yeye hatakwambia wewe ni nani, utakapofika pale.”

“Loo, endelea! Itanibidi kuliona,” akasema.

¹⁴⁹ Akaenda moja kwa moja Mbele Zake, labda kama huu, mstari wa maombi, popote pale. Yesu alikuwa akiwaombea wagonjwa. Basi Yesu alipomwangalia, mara ya kwanza aliyopata kumwona, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

150 Akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha mwalimu, “ulipata kuniona lini? Hii ndiyo mara ya kwanza niliyopata kukuona Wewe. Uliniona lini?”

151 Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.” Loo, ni jicho la jinsi gani!

152 Angalia ninii—angalia matokeo yake. “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Mtu huyo alijua. . .

153 Angalia tofauti kati yake na hao makuhani waliosimama huko nje. Hao makuhani hawakuamini, nao walijua lilitukia, kwa hiyo iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao. Kwa hiyo unajua walichosema? Walisema, “Anafanya. . . Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni Beelizebuli, pepo. Yeye ni pepo.”

154 Naye Yesu alisema, “Nitawasamehe hilo,” upatanisho haukuwa umetolewa bado, “bali Roho Mtakatifu atakapokuja,” sasa, “na kufanya jambo lilo hilo, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Kwa hiyo mnaona mahali lingetutupa kama tuliona jambo lile lile! Mnaona?

155 Sasa tunasonga mbele kidogo tu. Tunaona, basi, ya kwamba kuna matabaka matatu tu ya watu duniani, jamii tatu. Tunajua hilo. Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; hao ni Wayahudi, na Wasamaria, na Mataifa. Sasa, Msamaria ni nusu Myahudi na Mmataifa.

156 Sasa tunajua ya kwamba Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, sawasawa na Wasamaria. Bali sisi Wamataifa tulikuwa Waanglo-Sakson, tu—tuliabudu sanamu, tukibeba marungu mgongoni mwetu, na tulikuwa makafiri. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Wala hatukuonyeshwa Masihi yeyote, si hata ishara Yake. Tulinwona mtu akitembea, bali sio ishara ya Masihi.

157 Lakini kulikuwako na Samaria. Kwa hiyo Yesu, wakati mmoja akienda zake Yeriko, alizunguka mlima, “alikuwa ana haja kupitia Samaria,” basi akafika kwenye mji ulioitwa Sikari. Ilikuwa yapata alasiri, labda mahali kama hapa. Basi akaenda kisimani na kuketi chini, na—na kuwatuma wanafunzi waende wakanunue maakuli, chakula.

158 Basi walipokuwa pale, mwanamke, msichana wa mjini, kidogo mwenye sifa mbaya, alikuwa na waume wengi mno, akaja kisimani. Hakika, asingeweza kuja pamoja na wanawake hao wengine, maana, hiyo ingali ni desturi, hawawezi kuchanganyikana. Kwa hiyo akaja kuchota maji. Ndipo wakati alipoanza kuushusha m—mtungi wa maji, kwa winchi, achote maji, akasikia sauti ya Mwanamume ikisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Naye akaangalia kote, na huyo hapo Myahudi. Naye. . .

159 Hapana shaka alionekana mzee zaidi ya umri Wake. Hapana shaka alionekana mwenye umri mkubwa kidogo kuliko aliokuwa nao. Mwajua, walisema katika Yohana Mtakatifu 6 pale, kwamba, “Wewe ni Mtu asiyepata zaidi ya miaka hamsini, Nawe ulisema umemwona Ibrahimu? Tunajua sasa una pepo.” Akasema, “Ibrahimu asijakuwapo, Mimi Niko.” Kwa hiyo, lakini, Yeye, kazi Ya—Yake hapana budi ilimfanya aonekane kidogo labda ana mvi kidogo, ama kitu kama hicho. Alikuwa tu na yapata umri wa miaka thelathini na mitatu, lakini alionekana ni mzee kidogo.

160 Kasema, “Unasema, Wewe ukiwa ni Myahudi, unaniomba mimi mwanamke wa Samaria? Tuna ubaguzi. Hakuna kitu Wewe... Kamwe hatuwezi kufanya hivyo. Huwezi, hupaswi kufanya hivyo.”

161 Akasema, “Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema Naye, ungeniomba maji.”

162 Yeye alikuwa akifanya nini? Akiendeleza mazungumzo. Baba alikuwa amemtuma kule, bali alikuwa... Huyu hapa mwanamke; huo hapana budi uwe ndio wakati. Kwa hiyo akasema, alizungumza naye mpaka akaishika roho yake, akaona. Mnaona, Neno hutambua wazo lililo moyoni, Naye alikuwa ni Neno. Ni wangapi wanaoamini Yeye alikuwa ni Neno? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Mnaona? Nalo Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni. Mnaona?

163 Akasema, akapata shida yake ilikuwa ni nini. Sote tunajua ilikuwa ni nini; waume wengi mno. Akasema, “Nenda kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

164 Kasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye mumeo.”

165 Hebu mwangalieni maskini mwanamke huyo. Mnaona, alikuwa ameanguka kutoka kwenye mawazo ya Mungu. Angeweza kukombolewa. Alikuwa ni raia. Alikuwa na uwakilisho Mbinguni. Akageuka.

166 Angalia tofauti kati yake na hao wahubiri, makuhani wake. Hao wahubiri, wakati walipoona jambo hilo, walisema, “Vema, mtu huyu ni mpiga ramli.” Hawakujua Neno.

167 Angalia kile alichosema, “Tunajua. Bwana, hapana shaka wewe ni nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa mamia ya miaka. Nasi tunajua, Masihi ajapo, hiyo ndiyo atakayofanya.” Loo, jamani!

168 Angeweza—angeweza kuufundisha Birmingham jambo fulani. Angeweza kuufundisha ulimwengu wote jambo fulani. Naam, bwana. Angeweza kuzifundisha hizi seminari za kitheolojia jambo fulani. Mnaona? “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Angalieni, sisi...

¹⁶⁹ “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.” Mnaona, Yeye alisoma mawazo yaliyokuwa moyoni mwake. Akasema, “Hapana shaka wewe ni nabii. Tunajua, sisi Wasamaria. Tunamtazamia. Atakuja Masihi. Hatujakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne. Malaki alikuwa ndiye nabii wetu wa mwisho, naye alisema kutakuwako na mtangulizi. Tumesikia habari zake, mtu huko chini kwenye—kwenye Yordani kule, ‘Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia.’ Nimesikia habari zake. Nasi tunamtazamia Masihi kuja, mara moja.”

Kasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁷⁰ Hilo lilitosha. Huyu akaingia mjini, kasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Yamkini huyu Ndiye Masihi?”

¹⁷¹ Rafiki zangu, hatuna wakati wa kwenda mbele zaidi. Lakini kama huyo alikuwa ni Masihi jana, ni Masihi leo, kwa sababu Yeye ni yule yule jana, leo. Alikufa kusudi afanye upatanisho, kufanya mambo haya yatimie, kuwapa majaliwa ya kufaidika kwa yale aliyowafanyia. Sasa, kumbukeni, ikiwa wewe ni mwenye dhambi, kwa kweli uliokolewa wakati Yesu alipokufa Msalabani, bali inakupasa kuuamini na kuukubali kama wako, wokovu wako binafsi. Na kama wewe ni mgonjwa, uliponywa wakati Yesu alipojeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa kupigwa kwake uliponywa.

¹⁷² Sasa kama Yeye alikuwa amesimama hapa usiku wa leo, amevaa suti hii aliyonipa, kusingekuwako na... Kama ungesema, “Niponye, Bwana.” Asingekuponya. Tayari amekuponya. Mnaona?

¹⁷³ Lakini sasa vipi kama mtu fulani wenu akisema, “Je! Yesu angeweza kuwa Birmingham, basi, usiku wa leo?” Naam, bwana. Aliahidi angekuwa. “Angewezaje kuwa hapa, katika umbo la nini?” Roho Mtakatifu, hivyo ndivyo alivyo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuko katika umbo la Roho Mtakatifu.

¹⁷⁴ Sasa laiti ningalikuwa na wakati wa kuingiza wazo moja zaidi hapa, bali labda sitaingiza. Hebu, hebu nilipate, upesi sana. Mwaweza, mwaweza kuniruhusu dakika chache? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sitaki kuwachelewesha sana, na mkose mabasi yenu.

¹⁷⁵ Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu mlango wa 16, ama mlango wa 17, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Je! Yeye alisema hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁷⁶ Sasa angalia kilikuwa ni kitu gani. Yeye alikuwa akisoma Biblia ile ile tuliyokuwa tukisoma, Mwanzo 22 ama 19, 20, moja kwa moja hapo. Angalieni, alikuwa akisoma Biblia ile ile. Angalieni mandhari ya Lutu. Loo, lilikuwa taifa lenye dhambi jinsi gani, ni mahali penye dhambi jinsi gani! Angalieni tulilomo leo hii.

177 Angalieni kile Yeye alichosema, “Ki—ki—ki—kizazi chenye dhambi na cha zinaa; kizazi kiovu, cha zinaa kinatafuta ishara. Nao wataipata, ishara ya Yona akifufuka katika wafu; ama akiinuliwa kutoka katika hali sawia na kufa, katika tumbo la nyangumi kwa siku tatu mchana na usiku. Mwana wa Adamu, ishara ya ufufuo, kizazi hiki cha zinaa kingepokea ishara ya ufufuo.”

178 Sasa Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Angalieni mandhari. Kulikuwako na Malaika wawili kule chini miongoni mwa Wasodoma, wakihubiri, wajumbe wawili mashuhuri. Kuna Mmoja aliyekaa pamoja na Ibrahimu.

179 Na hao walioshuka kwenda Sodoma kule chini, walifanya ishara. Walifanya nini? Walihubiri Injili na kuwapofusha. Mahubiri yao yaliwafanya watu vipofu. Kama huyo hakuwa ni Billy Graham wa kisasa, sijapata kumwona mmoja. Hatujapata kuwa na mjumbe bado, katika nyakati zote, ambaye jina lake linaishia kwa -h-a-m, kwa kanisa. Kumbukeni, tumekuwa—tumekuwa na Moody, Sankey, Finney, Knox, Calvin, kadhalika, Billy Sunday, bali kamwe sio -h-a-m mpaka wakati huu; -h-a-m, “baba wa mataifa.” Yuko sasa, mnaona, kule chini. Angalia mandhari ya Sodoma.

180 Pia, kumbukeni, kuna Mtu aliyekaa pamoja nao kule juu, ambaye Ibrahimu alimwita *Elohimu*, Mungu. Angalia kile yeye, jinsi alivyojua kwamba Yeye alikuwa ni Elohimu. Alisema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.”

181 Umri wa miaka mia moja. Kasema, “Nitakuzuru, kulingana na ile ahadi niliyokupa, kwenye majira ya maisha,” siku zingine ishirini na nane. Ametazamia kwa muda wa miaka ishirini na mitano, sasa. Sara ana tisini naye mia moja. “Nitakuzuru majira haya mwakani.”

182 Ndipo Sara akafanya, “he-he,” moyoni mwake, hemani.

183 Akasema, “Kwa nini Sara akachekeka, hiyo ‘he-he,’ hemani, nyuma Yangu?”

184 Ibrahimu alimwita, “Elohimu,” Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa kibinadamu. Akila nda—ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, pia akila mkate, ugali; naye ni Mungu akijidhihirisha katika mwili.

185 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu,” wakati Mungu atajidhihirisha tena katika mwili wa kibinadamu.

186 Basi, kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho. Ibrahimu alikuwa ameona ishara baada ya ishara baada ya ishara. Lakini huyu hapa Mungu, wakati huu, akidhihirishwa katika mwili, na angeweza kujua kile Sara alichokuwa akiwazia,

nyuma Yake. Huyu alijua ilikuwa ni Neno, kwa kuwa Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni. Mnaona? Mnalipata? Inueni mikono yenu kama mnalipata. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Mnaona? Sasa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho.

¹⁸⁷ Sasa, kumbukeni, Ibrahimu na kundi lake hawakuwa Sodoma. Walikuwa nje ya Sodoma, si huko katika ulimwengu wa kimadhehebu; nje ya huko, huko nje. Mnaiona ishara waliyopata, jumbe kuu za kiakili? Lakini angalieni ni ishara gani Kanisa teule liliyopata, Ibrahimu. G-r-a-h-a-m ni herufi sita, ulimwengu, namba ya mwanadamu. Mwanadamu aliumbwa katika siku ya sita; yeye ni sita. Bali A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba, mnaona, Kanisa teule likisimama huko nje. Angalieni, waliipata ishara hiyo, Mungu akidhihirishwa katika mwili.

¹⁸⁸ Naye Yesu alisema, sasa angalieni, Luka mlango wa 17, katika ninii... “Itakuwa, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa.” Pia, kumbukeni, wakati Mwana wa Adamu, katika siku hizi za mwisho, anapodhihirishwa kwa watu Wake, kupitia nafsi Yake akifanya kazi miongoni mwa watu. Yohana, kama ilivyokuwa katika 14:12, ilisema, “Kazi nizifanyazo Mimi naye pia atazifanya.”

¹⁸⁹ Nasi tumeahidiwa hiyo, kurejesha. Kila sauti ina ujumbe nyuma yake. Nao Ujumbe ulikuwa, “Kurejesha imani kwenye Imani ya asili.” Malaki 4, “Kuirejesha Imani kwa... ya baba zao, kwa watu.” Wameenda kombo katika kila namna ya kila kitu, lakini, “Kuirejesha, tena, ile Imani.” Ujumbe wa wakati huu, ni “Rudini kwenye Neno!” Mungu, ninii...

¹⁹⁰ Kumbukeni, tunamtarajia Mwana aliyeahidiwa. Nasi ni uzao wa Ibrahimu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Uzao wa Kifalme, kupitia Kristo! Nao walikuwa wakimtazamia mwana aliyeahidiwa, Isaka. Nao Uzao wa kifalme, leo hii, tunaitazamia ishara iliyoahidiwa. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Mwana wa Mungu aliyeahidiwa, kurudi. Na ninii...

¹⁹¹ Walikuwa na kila namna ya jumbe, na Ibrahimu alikuwa ameona kila namna ya mambo. Lakini kabla tu ya yule mwana aliyeahidiwa, ile ishara ya mwisho kabla ya ulimwengu wa Kimataifa kuangamizwa, ilikuwa ni hii: Mungu akidhihirishwa katika mwili, aliyejua siri za moyo.

¹⁹² Sasa hiyo ndiyo ishara ya mwisho ambayo kanisa na Kanisa la kiroho hupata. Hiyo ndiyo ishara ya mwisho ambayo kanisa la kawaida linapata. Nao ulimwengu wa Kimataifa utaangamizwa, nao uko tayari kwa ajili ya jambo hilo sasa hivi.

¹⁹³ Dunia inatikisika kila mahali, kwa matetemeko ya ardhi. Kwa nini? Mara ya kwanza ambapo tetemeko la ardhi lilipoitikisa dunia nzima, ilikuwa kwenye Ijumaa Kuu. Mara ya mwisho lilipoitikisa, ilikuwa ni katika Ijumaa Kuu nyingine.

Kwa nini ilitikisika? Kwa sababu walikuwa wamemkataa Masihi wao. Kwa nini ikatikisika tena? Wamefanya jambo lile lile. Mnaona?

¹⁹⁴ Wakati wa Kanisa la Laodikia. Msomi yeyote anajua ya kwamba Yeye alikuwa nje, akibisha, akijaribu. . . “Tazama, nasimama mlangoni na kubisha.” [Ndugu Branham anabisha mara tano mimbarani—Mh.] Ndio wakati wa kanisa wa pekee uliowahi kumtupa nje kabisa. Nanyi Baraza la Ekumeni, hivyo ndivyo mmefanya hasa, kuifanya alama ya mnyama, na kuchukua mle ndani. Vema, ni kitu gani. . . Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana? Na kwa kufanya hivyo, wamelikataa Neno tena; Liko nje. Hata hawezi kupata ushirikiano, mahali popote. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁹⁵ Ee Mungu, uturehemu! “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁹⁶ Bwana Mungu, Wewe unajitambulisha Mwenyewe, katika nyakati zote, Mungu. Ulikuwa Mungu zamani za kale aliyenena na baba zetu kupitia manabii, katika siku hizi za mwisho kupitia Mwanao, Yesu Kristo; ambaye tunampenda na kumwamini, na kujua ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama alivyoahidi.

¹⁹⁷ Sasa, Baba, umati mzuri jinsi hii, imani nzuri. Ni rahisi kuwazungumzia. Lakini, Ee Bwana, jalia imani hiyo ipande juu tu sasa, iingie tu kwenye duara nyingine sasa, itoke nje ya mawazo ya kibinadamu. Wamesikia jambo hili. Wamefundishwa hivyo na wachungaji wao. Wao, wameitazamia, kwa miaka na miaka, ipate kuja. Na sasa tunaomba, Baba, kwamba utatujulisha, usiku wa leo, ya kwamba Wewe hujafa, bali U hai milele; na unaishi miongoni mwa watu Wako, kama Nyinyoro bondeni, miongoni mwa maua mengine yote, ua lililo zuri sana miongoni mwa elfu kumi.

¹⁹⁸ Sasa tunaomba, Ee Nyinyoro ya bondeni, kwamba utakuja kwetu, usiku wa leo. Jitambulisha miongoni mwetu, kujitambulisha katika wakati huu. Kwa kuwa imeahidiwa, ndio kwanza niwaambie Neno, kwamba katika siku za mwisho, kama Sodoma na Gomora, ndivyo Mwana wa Adamu atakavyojifunua Mwenyewe kama alivyofanya huko Sodoma na Gomora; kabla ya kuja kwa Mwana aliyeahidiwa kwa wateule, na maangamizi yakaja kwa waliokataliwa. Kwa hiyo ninaomba, Baba, kwamba watafahamu jambo hili. Basi naomba uje na kulitimiza Neno Lako, ambalo ninajua utalitimiza. Katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁹⁹ Sasa, ninaamini Billy alisema alisambaza kadi. Hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu kama kuna kadi zilizotolewa. Herufi iliyo juu yazo ni ipi? [Mtu mmoja anasema, “B.”—Mh.] B. Vema, B. Hebu tuninii upesi sana sasa. . .

200 Nitawaomba jambo moja, kama mtatulia tu kabisa sasa. Msisogee huku na huku. Tupeni tu dakika kumi. Mtafanya hivyo? Dakika kumi tu, kama kila mtu ataketi kimya kabisa kwa dakika kumi. Msisogee huku na huku. Vema.

201 Hebu tuanzie kwenye namba moja. Ni nani aliye na B, namba moja? Upesi sana sasa, inua mkono wako. Kama huwezi. . .

202 Mtu huyo aliyekuwa akienda kwa machela, angalieni namba ya kadi yake ya maombi ni ipi, kama ndiyo. Mnaona, je! una kadi ya maombi? Wewe, huna? Vema. [Mtu fulani anasema, “Ni nne.”—Mh.] Vema.

203 Namba moja, niliikosa? [Mtu fulani anasema, “*Hapa*.”—Mh.] Ama labda tutaanzia mahali pengine, basi. Vema. [Mtu anasema, “Papa hapa.”] Loo, nasikitika. Vema. Namba moja, namba mbili, tatu. Namba mbili, simama, maana. . . Simama wakati, wewe, nikiita namba yako. Mbili, moja, mbili, tatu, nne. [Mtu fulani anasema, “Papa *hapa*.”] Nne.

204 Tano. Angalia kadi yako sasa. Tano. Njoni papa hapa na mfanye mstari mdogo. Tano. Sita, sita. Saba, saba. Endapo huwezi kusimama sasa, acha mtu mwingine auinue mkono wako, tutawachukua. Vema, saba. Nane, nane, nane. Saba, nane. Sasa tunaninii tu. . . Kweli tunatumia muda wa ziada sasa.

205 Vema, hiyo ni sawa, mwache tu aketi hapo mpaka tutakapokuwa tayari kumwita, kisha tumweke tu mahali pake mstarini basi. Vema.

206 Tisa, tisa. Kumi, kumi. Kumi na moja, kumi na moja, kumi na moja. Achia hapo, basi. Vema.

207 Ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi, nanyi ni wagonjwa? Inueni mikono yenu. Vema, inueni mikono yenu. Ni wangapi hapa wasionijua mimi, inua mkono wako; anayejua kwamba sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako. Vema. Sasa angalieni upande huu na mwamini sasa. Mimi. . . Kila mtu awe na kicho sana.

208 Sasa kumbukeni tu, neno moja kutoka Kwake litamaanisha zaidi ya ninayoweza kuzungumza katika vipindi mia moja vya maisha. Mnaona, ningeweza kulihubiri Hili. Ni wangapi wanaoamini kwamba *Hiyo* ni Kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Sasa, kama ni Kweli, Mungu anawajibika. Kama hilo ni Neno Lake, hiyo ni ahadi Yake, Yeye anawajibika kufanya hivyo. Anawajibika kuthibitisha Neno Lake. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Na kama akifanya hivyo, mtaliadini? [“Amina.”] Liaminini.

209 Sasa unaweza kusema, “Ati Yesu? Siangalii huku na kumwona mahali popote.”

210 Angalia, vipi kama mtu fulani aliingia humu akiwa na makovu ya misumari mikononi mwake, na—na vitu usoni mwake mwote, na damu, na kadhalika? Mnafiki yeyote angeweza

kufanya hilo. Na, kumbukeni, Yesu hatakuja namna hiyo. Atakapokuja namna hiyo, hakutakuwako na wakati baada ya hilo. Hakutakuwako na wakati tena, wakati atakapokuja jinsi hiyo.

²¹¹ Lakini ungejuaje kwamba alikuwa Ndiye basi kama akija? Kwa kuwa angejitambulisha Mwenyewe kwa—kwa Roho Wake, ishara Yake, Maisha Yake ndani yako. “Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi.” Sasa kumbukeni tu na muamini hilo kwa moyo wenu wote sasa.

²¹² Sasa, huu ndio mstari wenu wa maombi, hao wote pale? Si—sijui, wanane ama kumi. Vema, hiyo ni sawa. Njoni hapa. Kesho usiku tutajaribu kuwachukua wengi zaidi. Kila mtu awe na kicho kabisa. Sasa waacheni tu waje, mmoja mmoja, wanapokuja.

²¹³ Sasa, kwanza kabisa, nataka wote walio kwenye mstari huo wa maombi, wanaojua siwajui, mstari mdogo wa maombi hapa, wanaojua siwajui, inueni mikono yenu; wanaojua sijui lolote kuwahuu, sijui lolote lenu, sijui shida yenu, sina fununu. Vema.

²¹⁴ Sasa, kwa kicho sana, sasa kumbukeni tu mahali tunaposimama. Neno limesomwa.

²¹⁵ Sasa, kumbukeni, siwezi kumponya mtu yeyote; hakuna mtu mwingine anayeweza kumponya mtu yeyote. Ila imani yako, katika kile Kristo alichio, ndiyo inayoponya. Sasa kama atajitambulisha Mwenyewe hapa kama alivyofanya, ajitambulishe jinsi hii kama alivyofanya katika siku zingine, mngeweza kumjua kwa hiyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivyo ndivyo tu alivyosema angejitambulisha Mwenyewe. Hivyo ndivyo tu alivyopata kujitambulisha Mwenyewe. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

²¹⁶ Kwa hiyo basi huyu hapa mwanamke, kama tu vile Yohana Mtakatifu 4. Yesu alikutana na mwanamke kisimani; ndio kwanza nimrejee dakika chache zilizopita. Huyu hapa mwanamume na mwanamke. Kamwe sijapata kumwona mwanamke huyu. Ndio kwanza ainue mkono wake, kwamba, sijapata kumwona wala yeye hajapata kuniona, kwa hiyo sisi hatufahamiani kabisa. Alipata tu kadi ya maombi, na ikatokea kwamba namba yake iliitwa. Je, ninyi. . .

²¹⁷ [Dada huyo anasema, “La, uliniombea huko Hammond, Indiana. Nilimaanisha, kwamba, hujui lolote kuhusu maisha yangu ya kibinafsi, hata hivyo.”—Mh.]

²¹⁸ Yeye alisema, wakati mmoja huko Hammond, Indiana nilimwomba, bali, kasema, kuhusu maisha yake ya kibinafsi, sijui lolote kumhusu, sijui lolote. Sijui upo hapa kwa sababu gani, wala chochote kile. Hakika, kuna mamia ya watu kwenye mistari ya maombi, ambapo huenda nimekuwa katika mikutano, na kadhalika, namna hiyo. Lakini ninamaanisha, kwamba, ninajua sininii. . . Mungu Mbinguni anajua, Biblia hii

ikiwa moyoni mwangu, nisingekumbuka hilo, mtu aliye mbali namna hiyo, mtu aliyeombewa labda miaka kadhaa iliyopita. Hammond, Indiana, hiyo ilikuwa ni muda mrefu uliopita, miaka mingi iliyopita wakati nilipokuwa Hammond, Indiana, miaka minane ama kumi iliyopita. Kwa hiyo sasa ninii tu. . .

219 Sasa kama Bwana Yesu atanifunulia ni nini kilichokuleta hapa sasa, hiyo ingefanya Yohana Mtakatifu 4 kweli kabisa. Lolote lililokuwa moyoni mwako, basi Neno hutambua wazo lililoko moyoni, kama Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Ungeamini kwamba hilo ni kweli basi? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Ungeamini?

220 Wasikilizaji wangeamini hilo kwamba ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

221 Sasa huu hapa mkono wangu juu ya Biblia, kwamba kamwe simkumbuki mwanamke huyu, nisingekuwa na fununu. Naye aliinua mkono wake, pia, nisingejua kile kilichomleta hapa. Alisema aliniona huko Hammond, Indiana, hiyo ingekuwa. . . Wewe—wewe, kila mmoja, huenda ulikuwa kule, ni juavyo mimi. Nisingejua, kwenye mkutano tu.

222 Lakini sasa Bwana Yesu na atujalie hili, akipenda. Sisemi kwamba atatujalia.

223 Sasa nachukua kila roho chini hapa, chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa iweni na kicho kabisa.

224 Ikiwa wewe si mwaminio, singekushauri ukae humu jengoni, maana magonjwa hutoka kwa mtu mmoja yakamwingia mwingine. Tunajua hilo. Vivyo hivyo na mateso. Wengi wamekuwa mikutanoni hapo kabla na kuona hilo likitukia.

225 Sasa ninataka tu kuzungumza nawe kama vile Bwana wetu alivyozungumza na mwanamke yule. Sasa, unaona, umesimama pale, mhitaji. Pia, wewe, labda u Mkristo. Sijui kama ndivyo ulivyo. Yeye ataniambia kama ndivyo ulivyo. Na, halafu, Mimi ni Mkristo. Sasa ni wawili, pamoja, mwanamume na mwanamke. Na, halafu, Roho wa Mungu yupo hapa na karama, kukujulisha unachomwambia, unachosema. Huenda ikawa ni mambo ya kifedha. Huenda ikawa ni mambo ya kinyumbani. Sina fununu yoyote. Lakini hata iwe ni nini, utajua kama ni kweli, au la, akilifunua.

226 Ni kivimbe. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa unaamini? Angalia sasa. Unataka nikwambie mahali hicho kivimbe kilipo? Kimo kooni mwako. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako namna hii. Sasa unaamini? [“Ndiyo, bwana.”] Vema. Nenda zako, ukimshukuru tu Bwana, kwamba una—unaamini hilo.

227 Njoo. Hatufahamiani, nadhani, mama. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Hatufahamiani, bali Mungu anatujuua sote

wawili. Unaamini Mungu anaweza kunifunulia shida yako? Ingekusaidia? ["Ndiyo."] Ikufanye uamini?

Iweni na kicho kabisa, kicho kabisa.

228 Sasa, kumbukeni, kulikuwako na mwanamke wakati mmoja ambaye hakupata kadi ya maombi, tutasema. Alipitia kwenye... akagusa upindo wa vazi Lake. Basi alipougusa, Yesu aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

229 Alikuwa anatokwa na damu. Akasema, moyoni mwake, "Kama ninaweza kungusa Mtu yule, nitaponywa." Naye akamgusa. Ndipo yeye...

Akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

230 Na, mbona, hata Petro alimkemea, kasema, "Hilo lingesikika kana kwamba ulikuwa na ugonjwa wa akili ama kitu fulani." Kasema, "Jamani! Mbona, kila mtu anakugusa."

231 Akasema, "Naam, lakini nimekuwa mnyonge. Ninaona kwamba nguvu zimenitoka." Akageuka na kuangalia kwenye wasikilizaji mpaka akampata mwanamke huyo. Ndipo akamwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa ni nini, kwamba kuliponywa. Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

232 Sasa Biblia ilisema, "Leo," hebu wahudumu watujibie hili, "kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa hivi anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli? [Wahudumu na kusanyiko wanasema, "Amina."—Mh.]

233 Wewe chukua tu kutoka Kwake. Useme, "Bwana Mungu, mhubiri huyo hanijui mimi. Basi nijalie kuligusa vazi Lako. Waweza kunena kupitia yeye?" Kama Yeye ni yeye yule jana, na hata milele, atafanya jinsi ile ile. Yeye yuko katika mwili wa kibinadamu sasa, akitenda, akiwakomboa watu Wake.

234 Sasa omba tu sasa, amini kwa moyo wako wote. Usitie shaka. Usishuku hata jambo moja. Amini mambo yote. Amini tu kwa kila kitu kilichoko ndani yako. Amini.

235 Sasa nataka kuninii tu—kuwasiliana tu na roho yako, mama, kuzungumza tu na wewe. Je! unaamini ya kwamba mambo haya ni kweli? Unaamini kwamba Bwana Yesu angeweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa? Wewe pia una kivimbe. Hiyo ni kweli. Unaamini Yeye anaweza kunifunulia mahali kilipo? Kimo katika tezi za kike. [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Na kwamba ni tezi gani, kiko kwenye tumbo la uzazi. Hiyo ni kweli. ["Ndiyo."] Vema. Amini sasa, nenda, kwa moyo wako wote uwe na imani.

236 Sasa huyu hapa mwanamume. Mwanamume siku moja alimjia Bwana Yesu, nalo jina lake lilikuwa ni Simoni, sasa, naye aliitwa Petro; Yesu alimwambia kwamba alikuwa ni nani na mahali alipotoka, ama kile kilichomhusu. Sasa kama Bwana Yesu anaweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa, utaamini

hilo? Unajua ingebidi iwe ni kweli, kama—kama unajua kama ni kweli au la. Lakini, wewe, unaamini mimi ni mtumishi Wake. [Ndugu huyo anasema, “Hiyo ni kweli. Ninajua hilo.”—Mh.] Unajua. Asante, bwana. Asante. Bwana na akusaidie sasa kuamini hilo kwa moyo wako wote.

237 Ni kitu hiki kidogo hapa, nilikuwa tu nikijaribu kukifanya kifungike vizuri. [Ndugu Branham anairekebisha maikrofoni—Mh.]

238 Sasa unapoangalia huku tena. Naam, bwana. Unapaswa kukabiliana na upasuaji wa henia. Hiyo ni kweli. Pia, ngiri, una ngiri. Je! Unaamini ninaweza kukwambia wewe ni nani? Unaamini? Wewe ni kasisi, wewe ni—wewe ni mhudumu, maana ninakuona mimbarani. Na jina lako ni Wallace. [Ndugu huyo anasema, “Ehe-ehe.”—Mh.] Amini kwa moyo wako wote. [“Utukufu!” Kusanyiko linashangilia.] Mungu akubariki. [“Hiyo ni miaka ishirini na miwili iliyopita, huko Pensacola.”] Vema, jamani, jamani! Vema. Kuwa na imani sasa. Usitie shaka. Kuwa tu na imani. Amini sasa.

239 Sasa hatufahamiani. Mungu anatumia sote wawili. Unaamini ya kwamba Bwana Mungu anaweza kuniambia jambo kukuhusu wewe, kile kilichokuleta hapa, ama kitu fulani? Kidogo ninaharakisha, kwa kuwa watu wa—wamesongamana, mwajua. Ni. . . Unaamini ya kwamba anaweza kunifunulia shida yako? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Unaamini. Nawe unajua hisi hiyo iliyokugusa, wakati uo huo, isingekuwa inatoka kwangu. Huyu ni Yeye. [“Ndiyo.”] Inakufanya ujisikie kabisa, kama utamu, unyenyekevu. [“Hiyo ni kweli.”] Na, Huyu, ulipata kuiona picha ya hiyo Nuru? [“Ndiyo.”] Mbona, Hiyo Ndiyo hasa inayokuzunguka sasa hivi.

240 Sasa mama huyu anasogea nyuma kutoka kwangu. Anaugua. Ninamwona, kidogo analemaa. Naye ana yabisi kavu, ambayo itaninii. . . [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”] Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. [“Ndiyo.”] Hiyo ni kweli. Halafu pia una ugonjwa wa kikoromeo. [“Hiyo ni kweli.”] Una ugonjwa wa kikoromeo. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli. Halafu una ugonjwa wa moyo, kusongwa kwa moyo wako. [“Ndiyo.”] Hiyo ni kweli, pia. [“Hiyo ni kweli.”] Hutoki hapa. Umetoka namna fulani ya nchi ambamo kuna ninii kwa wingi. . . Umetoka mbali sana. Umetoka Pennsylvania. [“Ndiyo, bwana, ndio.”] Hiyo ni kweli, ukashuka kuja hapa. Sasa nenda nyumbani ukapate afya. Yesu Kristo anakuponya, anakuponya.

Njoo. Kuwa na imani sasa. Usitie shaka.

241 Sasa msininii, msisogee, tafadhali msisogee. Kidogo tu sasa, tutaninii. . . kama mtanipa tu moja zaidi. Nipeni kisa hiki kisha tutamalizia, kama mtanipa tu kisa hiki. Msisogee, tafadhali msisogee. Najua ninawachelewesha sana. Lakini, mnaona, ninii

ni roho, nami ninawasiliana tu na kila mmoja wenu sasa. Mnaona? Sasa iweni na imani.

242 Ha—hatufahamiani. Sikujui mimi. Kristo anakujua.

243 Kuna mtu anayeshikilia kuja. Loo, ni huyu, m—mtu mwenye mvi aliyeketi hapa, akiumwa na magoti yake. Unaamini kwamba Mungu atakupa afya, bwana, na kukuponya, ugonjwa huo wa magoti? Nawe unaamini ya kwamba atakuponya? Mtu huyo aliye papo hapo nyuma ya ninii—kiti cha magurudumu pale, kama utaamini kwa ninii yote. . . Unaugua ugonjwa wa magoti. Inua mkono wako. Vema. Uligusa kitu Fulani, sivyo? Ulingusa Yeye. A-ha. Hiyo ni kweli.

244 Aisee, jambo lingine, mama huyo anayeketi hapo karibu nawe, nuru. . . mke. Unaniamini mimi, dada, kusudi wajue inatoka kwa Mungu? Unaamini kwamba mimi ni nabii Wake? Unaniamini mimi?

245 Huko ni kurudishwa mwangwi kwa hiyo. [Mfumo wa upazaji sauti una mwangwi wa mazingira sikizi ya jumba la mkutano—Mh.]

246 Unaugua shinikizo la damu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, weka mikono yako juu yake, pia, maana hakulipata vizuri sana. Halafu muamini kwa moyo wenu wote, nanyi nyote wawili mtapona.

Waligusa nini?

247 Hapa, mama mmoja ndio kwanza ashike hilo. Ameketi papa hapa nyuma, ameinamisha kichwa chake, akiomba. Anaomba Bwana amponye. Kile ananinii. . . Anaugua, ameketi papa hapa mwishoni mwa safu pale. Ana henia ya tumbo anayoombea. Nawe unaamini Mungu atakuponya, mama? Inua mkono wako. Maskini mwanamke yule mwenye nywele nyeusi aliyevaa miwani, ambaye alikuwa akiomba Mungu amponye. Simjui, sijapata kumwona maishani mwangu. Mungu anajua hilo. Kama hunifahamu mimi, pungu mkono wako, mama. Hiyo ni kweli. Sijui lolote kukuhusu. Vema, sasa, unajua ya kwamba hiyo ni kweli, sivyo? Vema, Yesu Kristo anakuponya, kama utaamini.

248 Aisee, anayeketi papo hapo nyuma yake, yule mama anayeketi pale, anayeketi papo hapo nyuma yake pale, yeye anaomba, pia. Ifuateni tu ile Nuru. Naam. Hivi hamwioni ile Nuru inayoning'inia moja kwa moja pale? Mnaona? Mnaona? Sasa angalieni. Mama huyo amefanyiwa upasuaji, bali kile anachotaka hasa Kristo amfanyie ni kuondoa donda ndugu mkononi mwake. Unaamini sasa kwamba Yeye atafanya hivyo? Inu- . . . Naam, inua mkono wako. Vema. Kama unaamini, unaweza kuupokea. Kuwa tu na imani, wala usitilie shaka. Amini. Mimi. . .

249 La, ni watu wawili mbalimbali. Niliwazia, mtu huyu; ni mtu *huyu* anayeketi hapa. Unaamini, bwana, unayeketi papa *hapa*?

Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini Mungu atakuponya ugonjwa huo wa tezi kibofu, akupe afya? Una ugonjwa wa tezi kibofu. Punga mkono wako, kama hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Imani yako inakuponya, bwana. Yesu Kristo alikuponya. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu.

²⁵⁰ Hivi hamwoni Yeye yupo hapa? Hivi humumwamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi hamwoni huyo ni Yeye?

²⁵¹ Sasa ngojeni tu kidogo. Ninii...Loo, naam. Siamini alikwambia lolote kukuhusu wewe binafsi, siyvyo? Unaamini anaweza kufanya hivyo? Unaamini ninaweza kufanya hivyo, kupitia neema na nguvu Zake? Itakuwa ni ahadi Yake? Unaugua ugonjwa wa shingo yako. Ulianguka, na hiyo ndiyo iliyoisababisha. Hiyo ni kweli. Rudi sasa, utakuwa mzima. Yesu Kristo anakupa afya.

²⁵² Mnaamini, kila mtu anaamini sasa kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa ni waaminio wangapi walio hapa? Inua mkono wako. Kote jengoni, juu. Vema, mnaamini. Sasa upesi sana. . . Kweli sisi, tumepitiliza saa karibu nusu saa. Fanyeni hivi sasa hivi. Yesu alisema. . .

²⁵³ Mnaamini Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaamini aliahidi kufanya jambo hili katika siku hii? Mnaamini ya kwamba hiyo ndiyo ishara ya mwisho ambayo kanisa hili litaona sasa kabla kuja kwa Bwana hakujatokea? Mnaamini tuko mwishoni kabisa, Maandiko yote yametimizwa, tayari kwa ajili ya kuja kwa Mwana?

²⁵⁴ Sasa Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa wewe weka mkono wako juu ya mtu mwingine aliye papo hapo karibu na wewe. Sasa, wewe ni mwaminio. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa kama Yeye hulitimiza Neno Lake, kufanya hivi, Yeye atatimiza Neno Lake kufanya hivyo, pia. Sasa wewe mwombe mtu aliye karibu nawe. Hao wanakuombea. Mnaona? Sasa usijiombe mwenyewe. Mwombe mtu huyo; wanakuombea.

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu sote tunapoomba.

²⁵⁵ Baba wa Mbinguni, tunashukuru kumwona Masihi aliyefufuka. Miaka elfu moja na mia tisa ya kila namna ya thiolojia na miondoko, bali hata hivyo, katika giza la hayo yote, Wewe uliahidi ya kwamba ungeonekana hapa katika siku za mwisho, katika siku hii ya Sodoma, Nawe ungejitambulisha kwa wana wa Ibrahimu, walioitwa, wateule. Nawe huyu hapa, usiku wa leo baada ya miaka elfu moja mia tisa, Wewe U hai usiku wa leo kadiri ulivyokuwa wakati ulipozungumza na yule mwanamke kisimani. Ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, sasa katika mwili wa Bibi-arusi Wake, kwa kuwa Bibi-arusi na Mumewe ni mwili ule ule. “Hawa wawili ni mmoja.” Nalo Kanisa linakuwa Bibi-arusi, wakati wote, kwa kuliamini

Neno, ili kwamba Neno na Kanisa linakuwa kitu kimoja. Neno katika Kanisa, likilifanya Bibi-arusi. Ishara ya mwisho, Mungu akijitambulisha Mwenyewe, lile Neno ndani ya Kanisa.

²⁵⁶ Ee Mungu, watu hawa wanaosema wanaamini, wamewekeana mikono. Wanaomba. Angalia chini kutoka kwenye Utukufu Wako, Bwana, tazama. Thibitisha Neno Lako. Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁵⁷ Ee Mungu, Shetani na apoteze mshiko wake katika imani yao usiku wa leo. Jalia Mungu aingie na kuwafanya wajue ya kwamba amejitambulisha Mwenyewe papa hapa miongoni mwetu. Nasi Yesu Kristo Mwana wa Mungu yupo hapa pamoja nasi sasa, Yesu Kristo aliyefufuka akatambulishwa, akijitambulisha Mwenyewe. Mara ya kwanza aliyofanya hivi tangu miaka elfu moja mia tisa iliyopita, Naye huyu hapa usiku wa leo. Shetani na apoteze nguvu zake; kutokuamini kwake kufifie, nazo nguvu za Kristo aliyefufuka ziingie ndani ya watu hawa na kumponya kila mmoja wao. Nasi tunamwondoa Shetani. Katika Jina la Yesu Kristo, na awaondokee watu hawa sasa hivi, ili wote waweze kuwa wazima; wakati wakiombeana, mmoja kwa mwingine, huku wamewekeana mikono. Tujalie, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁵⁸ Sasa endeleeni kuwekeana mikono. Aminini sasa. Endeleeni kuviinamisha vichwa vyenu, macho yenu yamefumbwa. Aminini. Sijali uko wapi, shida yako; hilo halijalishi. Kama Mungu, baada ya miaka elfu moja mia tisa iliyopita, amesimama papa hapa, akijitambulisha Mwenyewe, amefufuka kutoka kwa wafu; na kuchukua watu wapatikanao na mauti na kujionyesha Mwenyewe, Masihi katika nyakati zote, Masihi yeye yule akifanya jambo lile lile kwa ishara ile ile, Yeye amefufuka katika wafu. Aliahidi angefanya hilo kabla tu ya Kuja Kwake Mara ya Pili na kuangamizwa kwa ulimwengu wa Mataifa! Huyu hapa. Tutaliingilia kindani zaidi juma hili, tunapoendelea. Lakini wewe, kwa nini uteseke muda wote uliosalia katika juma hili, wakati unaweza kuponywa sasa hivi? Mtu fulani amekuwekea mikono, wewe. Mwaminio amekuwekea mikono yake. Yeye alisema Maneno haya, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya. Watapona.”

²⁵⁹ Unaamini kwa moyo wako wote sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama unaamini kwa moyo wako wote, na unaamini ya kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliyefufuka, Yule atakayekuhukumu kwenye ile Hukumu, yuko hapa usiku wa leo katika umbo na utu wa Roho Mtakatifu, na anajitambulisha Mwenyewe kwa ishara Yake ile ile ya Kimaandiko ambazo aliahidi kuwaonyesha, na kwamba Yeye alikuwa hai, Huyu hapa. Kama unaamini hayo kwa moyo wako wote, na kumkubali kama mponya wako, ninakuagiza, kwa Jina

Lake na kupitia Jina Lake, kwamba usimame kwa miguu yako sasa na kukubali uponyaji wako katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti. Simama, kama unaamini hilo. Simama.

²⁶⁰ Hilo ni sawa. Watu wanatoka kwenye machela, walitoka kwenye viti vya magurudumu. Na hilo ni zuri sana. Sasa mpeni tu sifa, kila mmoja. Inueni mikono yenu. Sasa ndio wakati mnapoweza kupiga makelele na kumpa sifa. Mnaamini? Kuna watu wametoka kwenye viti vyao vya magurudumu, kutoka kwenye machela yao, na kila mahali, wamesimama. Na tumpe sifa. Kila mtu inua tu mikono yako na kumsifu. [Kusanyiko linashangilia na kumsifu Mungu—Mh.] 

UTAMBULISHO WA KRISTO KATIKA NYAKATI ZOTE SWA64-0409

(The Identification Of Christ In All Ages)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 9 Aprili, 1964, katika National Guard Armory huko Birmingham, Alabama, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org